





**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**(CKRC)**

**Verbatim Report Of**

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, LIKONI  
CONSTITUENCY, HELD AT**

**LIKONI-MTONGWE SOCIAL HALL.**

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

[Redacted]

**OCTOBER 09, 2002**

**DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL, LIKONI CONSITUENCY, HELD AT LIKONI- MTONGWE  
SOCIAL HALL, ON 9<sup>TH</sup> OCTOBER 2002**

**Present:**

Com. Prof. A. I. Salim

**Secretariat Staff in Attendance**

William Opili - Asst. Programme Officer  
Gladys Osimbo - Verbatim Recorder  
Syria Lidodo and Ahmed - District Co-ordinators

The meeting started at 10.15 a.m. with Prof. A. I. Salim in chair.

**District Coordinator:** Nafikiri tutaanza sasa, na tutafuata desturi yetu ya kufungua kila kikao kwa dua, na kwa hivyo

ningependa lau mmoja wetu akaja hapa mbele na kutusomea jua ya kufungua kikao, .....(Inaudible), yuko? Hakuna mwenye kujitolea, nafikiri jamani, **Arabic**, nafikiri huyu jamaa mwingine .....(Inaudible).

**Speaker:** Shukran, *Prayer in Arabic*. Shukran.

**Com. Ahmed Salim:** Tutaanza kwa kuwakaribisha nyote kwenye kikao hiki cha Likoni Constituency. Mimi naitwa Ahmed Salim, mwana Tume katika ile Tume ya kurekebisha Katiba. Wenzangu hapa kwa upande wangu wa kulia ninaye Bwana Ahmed, ambaye ni District Coordinator. Na mkono wangu wa kushoto yuko mwenzake Sylvia na pale wako William na Gladys, sote twatoka kwenye kikao chetu cha Nairobi. Na madhumini ya kikao hiki kwa hakika, ni kutaka kueleza yaliyomo katika mswada wa Katiba mpya ambayo tumeandika. Mswada huu haujawa Katiba kwa hakika, lakini ni kama mapendekezo ya Katiba. Nitasema kwamba sisi baada ya kusikiza maoni ya wananchi kila pahali, tumeshikilia mapendekezo haya yaliyomo, katika mswada huu wa Katiba. Na kuthibitisha kwamba, mswada huu wa Katiba inafutia mia kwa mia maoni ya wananchi. Si mambo ambayo sisi wana Tume tumeandika tu, bila kufikiria wananchi.

Na kwa hivyo, tumefwata ile kanuni au ile sheria iliyo tuumba sisi kama Tume ambayo imetuambia kwamba baada ya kusikiza maoni ya wananchi, mtakaa, mtaandika mswada wa Katiba. Mtaandika report yenu au taarifa juu ya kazi mlioifanya tangu kuanza mpaka kumaliza au mpaka hivi sasa. Na kisha, mswada huu wa Katiba mtaeneza au kusambaza nchi nzima. Kuwe na vikao na wananchi kama kikao hiki. Mueleze wananchi mliandika nini katika mswada huu wa Katiba na katika taarifa yenu. Na kisha wananchi nao wawaulize maswala juu yake ikiwa hawa kufahamu au waseme kwamba hapa kuna hitilafu fulani, pia mngetia hivi na vile. Ndio ikiwa tumekuja hivi leo kufanya kazi hii ambayo ni stage inayofuata, baada ya kuandika ni kuisambazisha report yetu na pia mswada wa Katiba mpata kujua yaliyomo.

Wenzangu hivi sasa wako kila eneo Kenya kufanya kazi hii tunayo, ninayo ifanya mimi hivi leo na hawa wenzangu. Baada ya kufanya kazi hii kwa muda wa mwezi mmoja tu, tulianza tarehe ishirini na saba. Yaani, mswada huu wa Katiba ulikiamilishwa tarehe ishirini na saba mwezi wa September. Tuna mwezi mmoja kufanya kazi hiyo ya kuzambazisha *aleykum salaam*. Na baada ya hapo tutarudi Nairobi kujitayarisha, tafadhalini mtafika pale mjiandikishe kwanza kisha karibuni mkae.

Na baada ya hapo, mwisho wa mwezi huu tarehe ishirini na nane, tutatumai na nasisitiza, twatumai tutaweza kuanzisha ule mkutano mkubwa unaohusu Katiba, National Constitutional Conference. Mkutano ambao utawalata pamoja wajumbe mia sita na hamsini hivi. Wajumbe hao ni waakilishi wa wananchi wote nchini. Watakuemo Wabunge wote, watakuemo Commissioners wote sisi, watakuemo waakilishi watatu kutoka kila district ya Kenya, watakuemo viongozi wa kidini, kila dini iliyoko hapa Kenya na watakuemo waakilishi wa vikundi tofauti tofauti kama walemavu, vyama vya wafanyi kazi na kadhalika. Kina mama, waakilishi wao ili kuhakikisha kwamba kikao chao cha mia sita na hamsini na kadhalika, kitakuwa cha representatives, kinamwakilisha au kuakilisha wananchi wote.

Kila sehemu ya watu wa Kenya watakuemo waakilishi wao pale. Na madhumuni ya wao kukutana pamoja kwa muda wa mwezi mmoja ni kujadili au kujadiliana pamoja juu ya mswada wa Katiba. Waone yaliyomo na zaidi ya hivyo, kupitisha kila kifungu kilichomo katika mswada wa Katiba. Ikiwa kuna haja, baada ya majadiliano kubadilisha kifungu chochote watabadilisha. Yaani, huu mkutano mkubwa, National Constitutional Conference ndio kwa hakika utakao kata shauri kabisa na kwa njia ya mwisho kabisa. Na aina gani ya Katiba tutaipata? Kwa hivyo, hapa kuna mapendekezo kuhusu kila aina au kila hali ya maisha yetu. Aina ya Serikali tutakayo, aina ya wajumbe, mjumbe tumtakaye, aina ya mahakama tuitakayo na kadhalika. Kama mtakavyo soma baadaye. Kwa hivyo, na baada ya mkutano huo mkubwa, tafadhali kule nyuma kidogo mpunguze kelele nyuma kule tafadhali, registration, Shefa tafadhali na wenzako taratibu.

Mkutano huu ndio utakao maliza kazi ya Katiba. Baada ya mkutano huu mkubwa kupitisha mswada huu wa Katiba, tutaadilisha, tutaabadilisha, na baada ya kufuatia mazimio ya mkutano huo mkubwa. Final version itatolewa, itapelekwa mbele ya Bunge. Bunge ikipitisha, itakuwa ndio sheria yetu mpya. Kwa hivyo, hizo ndizo stages zilizobakia, tunafikia stage kumaliza stage ya mkutano mkubwa, na baadaye stage ya jumla. Kwa hivyo ningetaka kutumia wakati mrefu kidogo maana si nyote ambao nakala ya report yetu, au hata nakala ya mswada wa Katiba. Kwa hivyo ni muhimu mimi nieleze kwa urefu kidogo yaliyomo, kisha tutapata nafasi ya kuelezana zaidi na kujibu maswala yako.

Na kama nimesema kuna documents mbili, moja inayo mswada wa Katiba. Hii ni taarifa, report ya kazi yetu tuliifanya. Tulianza vipi tukatoka, ni maswala gani tuliuliza wananchi saa zile wakitoa maoni yao, na wananchi walisema kitu gani juu ya mambo gani. Na hii report kwa hakika ni fupi sana. Hii ni kama report au taarifa ya kifupi kabisa. Report yenyewe kubwa itakuwa ni mujalad au jalada tano, nne au tano, inategemea, haijamalizika. Na kwa hivyo, haijamalizwa kabisa, na kwa hivyo, na pia ni gharama kubwa kuieneza. Kwa hivyo tumefanya summary, tumeandika kifupi ili wananchi wapate kuisoma, na pia kuna taarifa hii imeandika kwa Kiswahili na Kiingereza. Sijui kama mlizonazo hizo copies ni za, ile ya. Kiswahili nasikia haijatolewa, lakini iko tayari na Mungu akipenda, siku hizi mbili, tatu, itakuwa tayari na copies zake zitafika kwenye kituo chetu kule Mombasa kwa akina Sylvia na Ahmed, ile library ilioko Mombasa. Nafikiri mwajua Sheikh Salim library inayojulikana zaidi kwa jina Sheikh Salim lakini sasa jina lake ni National Library Mombasa au tawi la National Library la Mombasa.

Sasa kwa hivyo bila kupoteza wakati maana tutakuwa muda, nitachukuwa muda mrefu kidogo kueleza yaliyomo, maana hamjapata nafasi tu kusoma. Tulichapisha kwa hakika mswada wa hii Constitution au Katiba katika Nation, Standard na the People, tarehe, ilikuwa tarehe ngapi?

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Ahmed Salim:** Tarehe mbili mwezi huu. Nafikiri wengine waliona, he?

**Audience:** .....(Inaudible).

**Com. Ahmed Salim:** Mliona na hamkuja na copies zenu, mngeweka mkaja hapa, mngekuwa ni rahisi zaidi kueleza. Hata hivyo, hebu nianze kueliza yaliyomo na baadaye tutapata nafasi kidogo ya kusikiza maoni yenu juu ya nitakayo waeleza kutoka hii Katiba iliyotayarishwa au mswada wa Katiba.

Mswada huu wa Katiba una suru ishirini. Umegawanywa katika sura ishirini au sehemu ishirini. Na inaanza na Preamble, kitangulizi. Preamble hivi sasa hatuna katika Constitution yetu ambayo tunatumia hivi sasa. Kwa hivyo tumeona kwamba ni muhimu kuwe na utangulizi au preamble katika Constitution yetu mpya. Preamble ni muhimu, kwa hakika ni fupi, kitangulizi ni kifupi lakini ni muhimu maana kinatoa fikra au wazo juu ya mapandeleo ya wananchi. Mapandeleo yao juu ya aina gani ya Serikali waitaka. Na kwa nini waitakayo serikali hiyo. Na yale maadili ambayo wao wangependa Serikali yao ya nchi yao ifuate. Maadhali ni mhimu kwa kile nchi. Yaani tuongoze, tufanye kazi kufuatia maadhili fulani. Maadhili ndiyo inayoweka uungwana nchini, mapenzi kati ya wananchi, umoja wao na kadhalika.

Kwa hivyo inasema, we the people of Kenya aware of our ethnic, cultural and religious diversity; and determining to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation; committed to nurturing and protecting the well-being of the individual, the family and the community within our nation and so on and so forth. Yaani, sisi watu wa Kenya, tukiwa twajuwa, kuwa sisi ni watu wa utamaduni tofauti, makabila tofauti, dini tofauti. Lakini juu ya tofauti hizo za kiutamaduni na kadhalika, na tukiwa tunapendelea kuishi kwa amani na umoja, kama dola moja, uma moja ambayo inajitawala yenyewe. Kwa kuwa pia tumekata shauri kulazimika kuishi pamoja, kumlinda mtu mmoja binafsi, kulinda familia na kulinda community nzima ndani, na uma wetu. Pia tukijua matumaini ya kila mwanamke na kila mwanamme katika kutaka kuwe na Serikali ambayo msingi wake na maadili yake ni uhuru, demokrasia, uadilifu wa kijamii, nafikiri tutafahamu uadilifu wa kijamii. Yaani sote ni jamii moja lakini kuna uadilifu kati yetu. Hakuna anaezajelewa zaidi ya mwenzaka.

And the rule of law, na hukumu ya kanuni, yaani, kuishi kufuatia kanuni. Kusiwe kuna watu kati yetu ambao hawafwata kanuni. Na pia, tukifuatia au kushikilia haki yetu, kukata shauri. Ni aina gani ya Serikali ambayo twaipenda. Na pia kwa kuwa tumeshiriki. Jambo hili ni muhimu. Tumeshiriki katika kuiandika Katiba yetu. Kwa kuwa tumeshiriki kuiandika Katiba yetu, sasa tumekata shauri kuikubali Katiba hii kujipa sisi wenyewe Katiba na pia kuwapa vizazi vijavyo Katiba hii. Hiki ni kitangulizi cha, na unamaliza kitangulizi kwa kusemal Mungu aibariki Kenya. Nafikiri tunakubalia Preamble kama hii, maana inasema wazi wazi matumaini yetu ni yapi, aina gani ya Serikali twaitaka, na kwamba sisi hii ni Katiba yetu tumeshiriki kuiandika na kwa hivyo tutailinda na tutaifuata.

Baada ya hapo tunaanza na sura ya kwanza. Sura ya kwanza ni fupi lakini ni muhimu pia. Inazungumzia sovereignty of the people and supremacy of the Constitution. Sovereignty of the people maana yake ni ufalme wa watu, yaani watu katika nchi ni kama ufalme. Ndio wanawakatiza hawo wamejua mambo ndio wanaosema wataka jambo gani? Na watu wale wengine tangu Rais mpaka yule messenger katika ofisi ya Serikali wote hao ni watumishi wa watu. Wamewekwa na watu, wamepigwiwa kura



na watu, wafanye kazi. Watu wasema twataka aina hiyo ya Serikali, fanyeni kazi, fwateni Katiba kwa kufanya kazi kufuatia Katiba.

Kwa hivyo sovereignty of the people, ufalme wa watu, and the supremacy of the Constitution pia ukubwa wa Katiba katika kanuni. Yaani, Katiba kwa hakika si kitu ila ni kanuni au sheria kubwa kabisa nchini. The Constitution is supreme, supremacy of the Constitution. Yaani kila mtu, kila mmoja wetu baadaye kama raia wa Kenya atafanya, hawezi kukosea Constitution. Na kanuni yeyote nyingine, ambayo iko katika vitabu vya kanuni itakuwa si halali ikiwa itagongana na yaliyomo katika Katiba. Na wakili wake yeyote kati yetu athibitishie katika korti kesho, kwamba huyu jamaa ameshikwa kwa njia isiyofwata Katiba, judge atakuwa hana budi la kumfungua maana Katiba ilivunjika, ilivunjwa na hatua ile iliyochukuliwa, tuseme na polisi au na mtu yeyote. Hiyo ndio maana ya supremacy of the Constitution. Constitution kuwa ni kanuni kubwa zaidi nchini. Na hiyo basi ni sura ya kwanza. Ni fupi lakini ni muhimu, ni kama *Alhamdi* katika Koran na ukubwa wake katika Koran.

Sasa sura ya pili yaitwa the Republic, Jamhuri. Katika Katiba yetu ya leo, kumetajwa kwamba katika laini moja nafikiri, kwamba Kenya ni Jamhuri, lakini hatuna maelezo zaidi ya hivyo. Kwa hivyo ni muhimu kujua Jamhuri ni kitu gani. Maana sisi wanatume tulikaa kwa muda mrefu katika kujaribu kuandika hii Katiba, kujadiliana juu ya mama ya Jamhuri ni nini. Nikiweza jiita Jamhuri ya Kenya, lazima kila mwananchi ajuwe maana kuwa Jamhuri ni kitu gani. Jamhuri ni neno la Kiarabu. Maana yake ni watu, raia, kwa hivyo nchi yetu ikiitwa Jamhuri maanake ni nchi ambapo watu ndio muhimu zaidi kuliko kitu chochote. Tuma raia kwa jumla ndio mhimu.

Na ingawa neno hilo Jamhuri limetokea neno la Kiarabu linaitwa Jamhur, lakini tangu hapo zamani, siku za Wagiriki, walipokuwa wakijitawala wenyewe walikuwa wakijitawala kwa kufuatia maadili ya kijamhuri. Maadhili baadaye yaliendelea, yakafwatua na Waroman, na tuweze kusema hata Waislamu pia walifuata, ikawa kila Muislamu nduguye Muislamu mwenzake ndio wako sawa. Tofauti iliyoko kuwa ni nani ambaye ni mzuri, nani ambaye amcha Mungu zaidi. Lakini otherwise, Muislamu halifa na Muislamu Waathi ni sawa, au siyo? Uislamu cha kuanza kabisa. Ndio litatumiwa neno hili linaitwa Jamhuri, kuwa watu wote ni sawa.

Kwa hivyo sisi tumekata shauri kwamba tutaendelea kuitwa Jamhuri ya Kenya lakini lazima kila mwananchi ajuwe kwa nini sisi twaitwa Jamhuri. Ndio nikasema tukakaa tukazungumza, tukazungumza, tukajaribu kueleza kwa nini kujiita Jamhuri. Tukasema kwamba Jamhuri hiyo yote au Jamhuri ya nchi yoyote iliyoitwa Jamhuri lazima iwe hiyo ni nchi ambayo itawekewa Serikali yake juu ya msingi kwa mambo fulani ambayo wataalam wa siasa au elimu ya siasa wanasema ndio msingi wa Jamhuri yeyote. Au maadili ambayo ni msingi wa Jamhuri yeyote, maadili gani? Utawala mzuri ambao wafuata siasa za vyama vingi, si chama kimoja kwa hii Jamhuri.

Pia maadili mengine ni utawala uwe unashirikisha watu. Ndio inaitwa Jamhuri, watu wanashirikishwa katika utawala ule. Ikiwa

si directly moja kwa moja, kwa njia nyingine. Kwa hivyo sisi tunashiriki katika kujitawala kwa njia ya election, siyo? Huyu tunampenda huyu hatumtaki. Huyu hakufanya kazi, kesho baada ya shughuli zetu tutamtoa, tutamtoa kwenye shughuli zingine ambazo ataahidi kwamba atatumikia. Na huyo pia atakuwa under notice. Atakuwa *Arabic* kwamba wewe usipofanya kazi yako sawa sawa utatoka, ataingia mwenyewe. Hii ni direct vilivyo. Lakini pia watu wanashirikishwa kwa njia nyingine. Kwa njia ya Parliament, maana wajumbe wetu kwa hakika ni wetu. Tumeweka wale, na hawo wajumbe Parliament, au Bunge pia itakata shauri ni nani atakaye kuwa Prime Minister, nani atakaye kuwa waziri. Nani atakaye kuwa balozi katika nchi hii na kadhalika. Maana mkisoma hiyo Katiba, utaona kwamba baada ya sisi kuwachaguwa wabunge, pia wabunge watukuwa na uwezo waku-approve kukubali au kutokubali appointment ya watu wakubwa wakubwa katika Serikali yetu na kadhalika.

Kwa hivyo maadili ya Jamhuri yeyote ni kwamba utawala uwe umeshirikishwa na wananchi. Pia maadili mengine, ya Jamhuri ni kwamba utakuwa transparent, ni wazi. Tunaweza kuona mambo yanayofanyika, tunaweza kuona jinsi mali ya wananchi inatumiwa. Tunapata hesabu kutoka kila idara, hesabu juu ya matumizi ya pesa zetu. Hiyo ndiyo Serikali iliyo wazi wazi tuweze kuona. Na accountable. Mtu afanya kazi utamwambia ati mimi nakupa, katika duka hili nakuwekea hivi na hivi na hivi, hebu nonyeshe, umeza kitu gani mpaka ngapi? Imebakia ngapi na kadhalika. Accountability, ufanyie mtu hesabu, mwenyezi Mungu kesho atakufanyia hesabu siyo? Kuna mazuri na mabaya, hiyo ni hesabu. Kwa hivyo Jamhuri huwa ni nchi ambao hesabu yake yajulikana. Mazuri yake yajulikana, mabaya yake yajulikana. Na wale ambao wanafanya vizuri wanasifiwa wanaendelea kutumikia nchi, lakini wale ambao hawafanyi kazi zao vizuri wanaadhibiwa. Maana kura ya wananchi kuna kanuni ambayo itamaliza. Basi hiyo ndiyo Jamhuri, na tukasema kwamba nchi yetu ya Kenya itakuwa ni Jamhuri.

Kesha tukasema kwamba lugha zetu kubwa zitakuwa ni mbili. Lugha za kirasmi zitakuwa ni Kiswahili na kiingereza kirasmii. Na lugha ya kitaifa itakuwa ni Kiswahili. Lakini pia tukasema kwamba Kenya hapo awali ni lazima kwamba Kenya, kuna watu wa kila kabila, kuna lugha nyingi, na tukasema katika mswada huu wa Katiba kwamba, lugha hizo nyingine lazima tujaribu kuziina, kuisadia, bado kusomeshwa na kwamba baadaye hatimaye kwamba schools au shule zitasomesha lugha hizo zingine tuseme, Kiluhya, Kiluo, Kikuyu katika zile classes za kwanza katika kila shule, maana hii Katiba kama nilivyosema ndio sheria kubwa lakini chini yake kuna sheria nyingine. Kwa hivyo education act .....(Inaudible) ya ile kanuni ya elimu. Itakuwemo mambo kuhusu kustawisha lugha zote za Kenya, ili kwamba mtoto wetu mdogo wa kila kabila ajuwe ile lugha yake au lugha ya mama yake, sawa? Hiyo ni sura ya pili.

Sura ya tatu ni muhimu pia. Sura ya tatu inaitwa National Goals Values and Principles. Shabaha za uma na maadili ya uma. Nafikiri sote twajuwa maadili ni kitu gani? Sasa sisi tukiwa ni uma au watu wa taifa la Kenya, maadili yetu ni nini? Tutafuatia mambo gani mazuri ili kwamba nchi yetu isitawike na tuishi tukiwa watu pamoja. Tunasema kwamba Serikali yetu itaendeshwa kwa njia iliyowazi. Wafanyi kazi wa Serikali watakuwa wenye kuhesabiwa. Tumetaja pia katika madhumuni ilivyo, au la? Lakini pia hapa tumetaja mara ya pili.

Pia tumesema ya kwamba Serikali ya Jamhuri yetu itaheshimu, italinda na kustawisha haki za kibinadamu na uhuru wa kila aina

ambao mwananchi atakuwa nayo kama haki zake za kuzaliwa. Maadili muhimu hayo, Jamhuri yetu itaheshimu, italinda na kustawisha haki zetu za kila mmoja wetu. Kila mmoja wetu hapa ana haki fulani. Kwa hivyo ni kazi wa wajibu wa Serikali kulinda haki hizo. Na pia tuna uhuru fulani. Uhuru katika maeneo mengi, uhuru wa kusema, uhuru wa kuzunguka katika nchi yetu ikiwa kwa amani bila nia mbaya. Bila kusimamishwa na kuambiwa wapi kipande na kadhalika. Uhuru wa kuchapisha, uhuru wa maoni ya kisiasa na kadhalika. Hizi ndizo uhuru tafauti ambazo kila mmoja wetu atasema kwamba anazo. Hakupewa na mtu, amezaliwa nazo. Na kwa hivyo tunasema katika maadili yetu ya Serikali yetu kwamba uhuru wetu na pia haki zetu za kibanadamu zilitalindwa na kustawishwa.

Pia tunasema katika sura hii, Serikali itajilazimu kuleta wadilifu wa kijamii na pia kumpa kila mtu haki zake za kimsingi. Uadilifu kijamii kama nilivyosema hapo awali, umuhimu wa uadilifu wa kijamii tumeeleza. Haki zake za msingi, kila mmoja wetu haki fulani, ana haja fulani, ana haja ya chakula, ana haja ya maji mazuri, ana haja ya makao, ana haja ya elimu, ana haja ya matibabu, ana haja pia ya mazingara mazuri kuishi. Hizo zaitwa basic needs, haja za kimsingi. Hakuna atakaye weza kuishi vizuri ikiwa hana mambo hayo, walahi. Kwa hivyo tunasema kwamba, Serikali itajilazimisha kuleta uadilifu wa kijamii na pia kuwapa watu haja zao za kimsingi.

Lakini pia tunasema kupumushoni kwamba mambo hayo yote hayawezi kutimizwa kesho na leo na kesho. Kuna gharama kubwa hapo. ....(Inaudible) Lakini tunasema kwamba, Serikali itaanza ....(Inaudible) hiyo kwa Katiba na itaendelea. Lakini hatuweki kiwango cha muda. Itakuwa ni kazi ambayo itafanyika, na saa zote ikichunguliwa. Pia tunasema, kwamba maajili mengine yasema kwamba maendeleo na ustawi utasambazishwa katika kila eneo. Hayo ni maagizo mengine. Katika kuzunguka na kutoa, kupokea maoni kwa wananchi kulikuwa na malalamiko hapa na pale, kwamba area yetu hii haitizamwi. Tunalipa kodi lakini bara bara ni mbaya, hatuna hospitali, hatuna matibabu, hatuna hivi, shule hazitoshi na kadhalika.

Pia kuna factory yetu hapo ilikuwapo ikiwa pa watoto wetu, lakini sasa imefungwa. Kwa hivyo sasa tunasema kwamba maadili yetu ni kwamba maendeleo na ustawi uatagawanywa katika kila eneo, ili kila mmoja atafaidika sawa na mwenzake katika eneo hili. Hiyo ndio sura ya tatu.

Sura ya nne yahusu uraia, wananchi au uraia. Nani raia wa Kenya? Tunasema kwamba kwanza raia wote ni sawa. Hakuna raia mmoja ambaye ni bora kuliko mwenzake. Pia wajibu wa raia mmoja ndiyo wajibu wa raia mwengine. Ukisikia hao wengine wanaambiwa lazima ufanye hivi na vile lakini yule mwingine anaambia wewe hakuna haja ya kufanya. Kuwe usawa kati ya raia. Ukisha juwa kwamba huyu ni raia wa Kenya na huyu ni raia wa Kenya, hawa wawili ni sawa sawa. Hakuna mmoja ambaye ni bora kuliko mwenzake.

Pia tunasema kwamba mtu atajulikana kuwa ni raia ikiwa mzazi wake mmoja ni raia, si lazima wote wawili wawe ni raia. Ikiwa baba ni raia na mama si raia, yule mtoto atakuwa ni raia. Ikiwa mama ni raia lakini baba si raia, mtoto pia atakuwa ni raia. Pia ikiwa mama ataoa nje, atakuwa na baba mgeni, yule baba pia apate uraia wa Kenya. Kwa hivyo sasa akina mama ambao

huowa nje mume huwa hapati uraia, lakini ikiwa mme aowa nje, mkewe apate uraia. Kwa hivyo tumeondoa ubaguzi huu kati ya mwanamke na mwanamme, wawe wote sawa. Yeyote atakaye muoa mtu ajinabi kutoka nje yule atakaye olewa, au atakaye oa atakuwa ni raia wa Kenya, tuna fahamiana? Kwa ufupi lakini kuna mengine ambayo yametajwa kuhusu uraia lakini kwa kuwa hatuna wakati na mswada huu ni mrefu, nitapata nafasi kuwaeleza pole pole, lakini kama tukipata nakala za kutosha, tutazisambazisha. Tutakuwa na nakala za kutosha kwenye kikao chetu cha ofisi yetu hapa mjini, tuweze kusome kwa urahisi.

Kisha tunaingilia sura ya tano ambayo ni .....(Inaudible), hii yaitwa the Bill of Rights. Kila nchi ambayo ina ustaarabu wake lazima iwe na .....(Inaudible). Kunayo Bill of Rights tukitaka. Lakini tulilifanya ni kustawisha zaidi, kufanya bora zaidi ili kwamba kila mwananchi ahisi kwamba amepata haki za kutosha. Mimi si mtaalamu wa mambo hayo ya Katiba, lakini wenzangu katika Tume, wamesema kwamba hii Bill of Rights chapter hii au sura hii, ni ndifu na yana mengi zaidi kuliko sura za Bill of Rights za nchi nyingi za ulimwenguni. Hiyo ni kwamba kwa kuwa tumesema kwamba mwananchi wa Kenya aishi kwamba anahaki na ajuwe haki zake na kwa njia hii apate demokrasia kubwa zaidi katika nchi yetu.

Na pia ni ndefu kwa hivyo sina wakati wa kusoma haki zote, lakini niseme kwamba inasema hapa kwamba Serikali itachukuwa hatua za kuweka sheria zinazohitajika kuwapatia wananchi haki za kimsingi kama nilivyosema. Chakula, matibabu, elimu ya msingi, maji masafi, makao, na amani ya binafsi. Tunalalamika saa zingine tukizinguka watu wanasema, tunasimamishwa njiani, tunaingiliwa, polisi wako wapi, tunaita hawaji na kadhalika. Ili amani ni lazima istawishwe zaidi katika nchi yetu kwa kila mwananchi ahisi kwamba alitoka, akilala, akifanya kazi, hali yake ni ya amani.

Haki nyingine, kusiweko ubaguzi wa kikabila wa jinsia, uasili, wa rangi, wa umri, wa uzima, juu ya yule ambaye ni mlemavu na wajane au wa utamaduni, au lugha. Watu wote ni sawa. Tuzizingatie kabisa, iko lugha yake, utamaduni wake, ikiwa ni mwanaume, mwanamke, ikiwa ni mzima au mlemavu, ikiwa Muislamu au ni Mhindu au ni Mkristo, sote ni sawa. Kusiwe na ubaguzi wowote, tukiwa sote ni pamoja ni watu na raia wa nchi moja.

Tatu, haki za wazee. Tumezungumza hapa na pale, na wazee wengi wamesema kwamba wanapata taabu, hawana maisha mazuri, wakipata kufika uzeeni wanasahauliwa na kadhalika. Kwa hivyo, tumeweka hapa aina ya sheria ambayo utakuwa ni wajibu wa wazee, watoto, ni wajibu wa jamii, na pia wajibu wa Serikali kuhakisha kwamba wazee wetu, our senior citizens wana retire katika kazi zao na wanapata maisha ambapo wana hisi kwamba wanapata chakula cha kutosha na makao ya kutosha. Lakini, hiyo itakuwa ni kazi ya uma nzima, watu wote, Serikali na wananchi wote.

Pia haki za watoto, tumezungumzia katika hii Bill or Rights. Watoto kulelewa vizuri na wazazi, kuvishwa vya kutosha, kuelemeshwa, kutolazimishwa kufanya kazi. Kuna wazazi huwa wanalazimisha watoto lakini kwa kuwa kunaweza kuwa labda kuna upungufu wa chakula nyumbani, hakuna mapato ya kutosha, ama unaambiwa mtoto nenda pale duka la fulani ukae na vituambua hivi na mahamri ueze. Badala ya kupelekwa skuli. Saa zingine huwa hakuna haja ya kufanya hivyo. Kwa hivyo watoto lazima walindwe na kutopewa haki zao. Kila binadamu kuanzia utotoni ana haki fulani, kujistawisha nafasi yake. Kwa

hivyo ni haki ya wazee kutojifikiria nafsi zao, na kuwafikiria watoto kwa wale si wana haki zao binafsi. Lakini wajibu wa wazazi ndio na Serikali kuwapa haki hizi za kuelewa na kulishwa. Na wasitumiwe vibaya, wasipigwe ovyo, wasitumiwe vibaya pia. Sina haja kutaja mengi nafikiri kila mmoja wetu anajuwa hali zilizoko. Matamshi mabaya ya watoto kwa njia mbaya saa zingine. Hapa hapa nchini na pia na hawa watalii ambao wanakuja. Kwa hivyo mambo kama hayo lazima tuyafikirie.

Pia haki ya walemavu. Haki ya walemavu kuwa ni sehemu ya nchi yetu na wana haki ya kupata makazi ya kutosha. Katika mswada huu tunahimiza matajiri kuwapatia kazi sehemu fulani katika kazi zao, wapatie walemavu.

Pia tunahimiza majengo makubwa yatumie lift ili kwamba mlemavu aweze kufika anapotaka kule....(Inaudible). Sasa ukifikiria, ma-ofisi mengine makubwa huwa ni shida sana kwa walemavu .....**(Phone interruption)**.

Poleni sana, pia privacy. Mtu ana haki, nyumba yake Waingireza wanasema nyumba ya mtu ni kama castle, kama ngome, ngome yake, lazima ilindiwe na isishambuliwa na mtu. Kwa hivyo privacy ya kila raia ni muhimu, asiingiliwe nyumbani wakati wowote ambapo mtu atakapo kumwingilia. Askari wanakuja wanavunja mlango wanaingia ndani, wanaanza kumpekeshini mambo yake .....(Inaudible) kwa hivyo tunasema kwamba, haki ya raia kulindwa na haki ya mali yake, lazima yaheshimike.

Lakini tunasema pahali pengine katika maelezo kwamba, hutokea wakati mwingine kwamba ikiwa ni mtu ambaye anashukiwa na kuna shaka ya kutosha. Basi lazima ithibitishwe kwamba hapa kuna haja ya kuingia hapa na kupekisheni nyumba hii popote tumesikia kwamba kuna hili au lile. Lakini katika hali kuwa mtu yeyote ataingiliwa wakati wowote, iwe si sawa, na hiyo ni kuvunja haki ya mwananchi.

Tunafikiria pia tumezungumzia familia na haki zake. Haki zingine pia, zinasema kwamba zile zote ni sawa katika nchi yetu Kenya. Kenya haifwati kirasmii dini yoyote, Kenya si nchi ya kikristo, Kenya si nchi ya kiislamu, lakini haki za dini zote na watu wanaofwata dini zote wanahaki ya kufwata dini yao bila ya kuingiliwa. Na kila dini ina haki ya kuendesha haki zake na watoto, wafuasi wa dini hiyo wanahaki kusomeshwa katika dini hiyo.

Pia hakuna ruhusa ya mtoto wa dini fulani kulazimishwa kufuata dini nyingine. Kwa sababu yeyote. Kwa hivi sasa tunaambiwa kwamba mtoto akiingia skuli fulani ni lazima asomeshwe dini ya waliobuni skuli ile. Hiyo sasa imekataliwa. Mkristo akiingia katika shule ya Kiislamu, asilazimishwe kufuata dini ya Kiislamu. Muislamu akitaka kuingia katika shule ya Kikristo asililazimishwe kufuata ibada ya Kikristo na kadhalika. Kila mtu ana haki, na analindwa haki yake kufuata ile dini ambayo akitaka yeye bila kulazimishwa kwa sababu .....(Inaudible). Na pia siku zile za rasmi za kuabudu lazima aruhusiwe ajipange aende atoe au afanye ibada yake atakayo, swala ya zetu za kiislamu.....(Inaudible).

Religious observances and religious instruction may be conducted at state or state headed institutions so long as they are

conducted in an equitable basis so that no religion is privileged. Hakuna dini ina umuhimu zaidi ya dini nyingine. Dini zote ni sawa. Ikiwa kwa mfano tumepata ushahidi kwamba dini fulani inapendelewa zaidi, mtu anaweza kushitaki kwamba jambo hili ni dhidi ya Katiba.

Freedom of Expression, haki ya kusema kama nilivyosema. Mtu ana haki ya kutoa maoni yake, bila hofu, lakini, asiseme mambo ambayo huenda yakaleta mvurugano. Akaanza kutukana nyinyi fulani. Hapo ataleta magombano kwa vijana na pia mtu akauwawa au watu wakauwawa. Kwa hivyo, haki hii ina mipaka yake. Utasema mambo ambayo ni right yako lakini si kutukana, si ya .....(Inaudible).

Haki ya kujumuika pamoja. Mtu ana haki kujumuika na wenzake kuhusu jambo lolote. Bila kuingiliwa ukaambiwa wewe huna haja kukutana, au huna haja, au mkutano huu ni si wa halali.

Pia kutoka katika demonstration kuna haki ku-demonstrate, maadam tuna-demonstrate kwa amani bila kuanza.....(Inaudible).

Freedom of movement and residence: E very person has the right to freedom of movement. Kama nilivyosema hapo awali mtu asiwe na haja ya kukusimamisha, kukuwambia unakwenda wapi? Wewe ni Kenya, atakupeleka, polisi akakufungia, mambo kama haya ndio yanayo .....(Inaudible) na kadhalika.

Social security kama nilivyosema amani ya kijamii. Every person has the right to social security. Including if you are unable to support yourself, and the independence appropriate social security .....(Inaudible). si wazee tu lakini mtu yeyote mwenyewe, ambaye hali yake ni zaidi, hawezi kujisaidia mwenyewe, hana chakula cha kutosha. Ni wajibu wa Serikali kutafuta njia ya kusaidia, lakini tuliposema kila nchi ina njia yake ya kufanya. Ukienda kule America, wale ambao hawana mapato mazuri wanafaa .....(inaudible) akiingia kwenye supermarket anaweza kuchukuwa vitu hivi maadam ile  
\$ End of side A

.....Kwa watu wanaofanya msaada, wanapata, na hakuna atakaye juwa, ila yule ambaye yuko nyuma yake kwamba huyu, maskini, hajiwezi kwa hivyo amesaidiwa na serikali na kadhalika. Samahani kuna mengi lakini kama nimesema baadaye mtajisomea wenyewe kwa urefu zaidi haki zingine ambazo hatukuweza kuzitaja.

Pia yule aliyeshikwa, mshitakiwa, katika kushikwa lazima apewe treatment ya kibinadamu. Ya kiuatu, ya kiunguwana, asishikwe bila kuulizwa kama baado hajaingizwa kwenye cell asha pigwa, ashatokwa na madamu na kadhalika. Hayo sasa tumeyakataza kabisa katika kortini. Atawekwa, atapewe chakula wakati wa chakula, atapelekwa kortini wakati kortini, apewe haki ya kupata wakili ikiwa hajiwezi kumtetea na kadhalika.

For fair trial. Kuhukumiwa kwa njia ya uadilifu. Sura ni ndefu hiyo, na kwa mengi, na ni mhimu sana. Bill of Rights, hii utaendelea, sawa sawa?

**Speaker:** Yaah, Yaah,

**Com. Ahmed Salim:** Ooh,

**Speaker:** .....(Inaudible) because of the tribute, .....the generator.

**Com. Ahmed Salim:** But this is affecting the recording, samahani tungojea maana tuna nasa tuna nasa kila neno, na noise, na .....(Inaudible)

**Audience:** .....(Inaudible).

**Com. Ahmed Salim:** Can you stop, they are disturbing.

Sura ya sita inaitwa uakilishi wa watu, representation of the people. Uakilishi wa watu katika Bunge na hapa tunumzia mambo ya uchaguzi. Tunasema kwamba, uchaguzi utakuwa kwa secret ballot, uchaguzi, kura ya siri. Nimesema kwamba kutakuwa na continuous registration of voters, mambo hayo yalisemwa sena. Wananchi wakisema kwamba haitoshi kwamba tungojee mpaka watu watuambie kwamba kwa muda wa mwezi mmoja tutafanya registration lakini iwe ni saa zote, mtu atakapo jiandikisha kuwe na ofisi fulani ambapo anaweza kuenda akajiandikisha kwa ajili ya kura. Na pia tunasema kwamba hapa tunaanza kuingilia mambo kuwasaidia akina mama kuhusika katika mambo ya maisha yetu ya kila aina, hapa maisha ya uiwakilishi. Kwamba akina mama theluthi ya wale ambao watajiweka mbele ili wachaguliwe, wapigiwe kura, theluthi iwe ni kina mama. Na kwamba hamsini katika wale ambao tutawapa, nitaeleza baadaye, kutakuwa na viti aina fulani mbali na mia mbili na kumi vya Wabunge, kutakuwa na tisini wengine. Hao tisini, watachaguliwa na kugawanywa au viti hivyo tisini, vitategemea idadi ya kura ambazo kila chama kitapata. Tusema KANU, kura zake zote zitajumulishwa, DP kura zake zote zitajumulishwa.

Kila chama, kura zake zote zitajumulishwa, na kisha itatumiwa formular au njia ya kupata ile idadi ambayo kila party itapata ya viti hivyo, na viti hivyo sitini vitagawanywa kufutia idadi ya kura ambayo kila party itapata. Tuseme KANU ikipata kura .....(Inaudible) watapewa viti zaidi ya viti vile vile ambavyo nafasi hiyo kwa njia ya election ya desturi ile haja. Sijui kama sikueleza vizuri hapa nafikiri. Yaani hivyo tisini ni kama reserved hizo. Kisha vitagawanywa hivi tisini kati ya party zote zilizo shiriki katika uchaguzi. Na kila party au kila chama kitapata sehemu kufuatia idadi ya kura ilizopata siyo?

Yaani, hivi ni kuhakikisha kwamba kutakuwa na demokrasia zaidi katika nchi. Yaani, tutafanya hivi maana yake ni kwamba ni kura nyingi zitapotea. Na wananchi wengi kura zao zitapotea, hazina mtu wa kuakilisha. Tuseme katika hapa Mtongwe,

kutakuwa na jamaa wawili watakao pigania kiti cha Likoni niseme, okay. Sasa ikiwa mmoja anamshinda mwenzake kwa kura kumi tu au kura tatu, itakuwa maanake yule aliyeshindwa, kura zake zote zile zilipotea. Na kwa nini tunasema kwamba kura zile za yule aliyeshindwa, ziende katika kura za chama chake. Na kwingine pia, kura za mwenzake katika chama kingine ambaye ameshindwa, pia ziende kule, na yule aliyeshinda pia kura zake zitawekwa kwenye kura za chama chake. Kwa hivyo kila chama kitakuwa na idadi ya votes. Na kufuatia idadi ya kura, kile chama kilichopata watapewa sehemu fulani katika zile tisini zaidi. Na kwa njia hii maanake ni kwamba raia pia aliyepiga kura, amepata muakilishi kule. Tumeona kwamba system hii, au mpango huu, wakupata uakilishi Bungeni ni bora zaidi na wakidemocrasia zaidi.

Pia tunaeleza ni nani ambaye ana haki ya kusajiliwa kuwa mpigaji kura. Sisi pia tunazungumza juu ya electoral commission na kazi zake, tunasema kwamba electoral commission sasa ndiyo itakayo kuwa na jukumu, tuko na maamlaka au jukumu ya kusajili vyama vya kisiasa. Hivi sasa vinasajiliwa na registrar wa society. Tunaona kwamba kule registrar wa society ahusike tu na hivi vya welfare na kadhalika na ma-NGOs lakini vyama vya kisiasa, viandikishwe kwa electoral commission. Pia electoral commission itasimamia uchaguzi wa kila chama. Chama kikiwa na siku ya uchaguzi wake, kusema ni nani secretary general, nani chairman, nani treasurer na kadhalika, pia electoral commission, kwa kuwa ni neutral body isimamie.

Pia kila chama kitakuwa na wajibu wa kuweka hesabu mapato yake. Donations kutoka kwa wanachama, donations kutoka nje na kadhalika. Na hesabu hiyo kila mwaka itapelekwa kwa auditor general na report. Pia kila chama ambacho kinapata sehemu fulani ya kura kitapewa msaada kutoka kwa Serikali kipate kuendelea na kazi zake. Lakini chama ambacho kwa muda wa uchaguzi mbili, hakikupata kiti chochote hicho kitaondoshwa, maana chaonyesha kwamba hakina watu kuwapatia na kadhalika.

Kisha tunaingilia sura ya legislature yenyewe, Parliament. Hapa pia tumezungumzia mabadiliko au tumetoa maoni juu ya kubadilisha mambo kidogo. Tumesema kwamba Parliament sasa itakuwa na vyumba viwili, two houses of Parliament, Lower House and Upper House, au National Assembly na National Council. National Assembly ni hii tulionayo sasa. Lakini kama vile nimesema kutakuwa na wale mia mbili na kumi na tisini wengine. Kwa hivyo National Assembly itakuwa na Wabunge mia tatu, sawa? National Council hiyo ni mpya. Hiyo ndio Upper House au baraza la wazee mkitaka kusema. Lakini inaitwa, National Council. Sasa kutakuwa na wajumbe tisini, la mia moja. Sabini wakuwa ni district representatives, kila district Kenya kuna sabini. Itakuwa na mjumbe mmoja, kwa njia ya uchaguzi. District itakaa, kutakuwa na election kwa ile district atapelekwa mjumbe mmoja, hao ni sabani. Kisha kutakuwa na thelathini, au viti thelathini ambavyo vitakuwa special kwa kina mama. Jumla viti mia moja.

Kwa nini tumetaka kuwa na nyumba mbili za Parliament? Tunaona kwamba kwa njia hii kutakuwa na pia democrasia bora zaidi. Pia mambo yataendelea bora zaidi. Saa nyingine utaona kwamba Parliament hii tuliyonayo hivi sasa inapitisha kanuni ambazo saa nyingine sijui kama nasema sawa, wajamaa wengine wafikirie kwamba imepelekwa haraka, haikufikiriwa uzuri, na kadhalika. Ndio ikawa nchi nyingine kama America pia wana nyumba mbili, House of representatives and Senate. Pamoja



hawa wanaitwa congress, American Congress, siyo? Saba ni kwamba kanuni au mswada wa kanuni ukipelekwa katika nyumba moja, na kupitishwa, na ukipelekwa kwa nyumba nyingine, pale unapata nafasi ya kufikiriwa zaidi kujadiliwa zaidi. Na huenda ikawa ni kanuni bora, imeanza kufikiriwa hivyo. Na jambo hilo limejaribiwa kwingine, UK pia Uingereza, kuna House of Commons and House of Lords. Kanuni ikishapitishwa, House of Commons, inapelekwa House of Lords inajadiliwa. Na mara nyingi ikifika House of Lords, pia, katika majadiliano katika House of Lords, utaona kwamba wanatoa maoni mazuri saa zingine. Ikawa ile sheria itabadilika. Ingekuwa haifai House of Lords, ingeondolewa, ikiwa ni hasara.

Lakini utaona kwamba mabadiliko yako, yanaandelea kule Uingereza juu ya House of Lords, wataka ondosha ile siasa kwamba members of House of Lords ni wale matajiri au wale ambao babu zao na babu za babu zao walikuwa ni matajiri wa zamani, waliyoiba mashamba na kadhalika, wakapata utajiri wa kirongo. Tawa taka sasa iwe ni more representative, iwe ni house au ni nyumba ambayo wamo waakilishi wa watu zaidi, more representatives. Lakini hiyo ni mbali, muhimu ni kwamba, imebakia, .....(Inaudible) na inafanya kazi nzuri. Sisi tumeambiwa kwamba, si hasara lakini jana kikao chetu kule Changamwe tuliambiwa kwamba, nchi yetu inaweza kustahimili gharama ya kuwa na two houses. Kweli itakuwa gharama kubwa, another house and some one hundred other members walipwe mishahara na kadhalika. Tukasema kwamba hili ni pendekezo, katika ile National Conference ambayo nimeitaja hapo awali, bado itazungumzia, na sisi tumeona kwamba kuna faida hapa. Na ikiwa wakilishi wetu katika National Conference watafikiriwa, watajadiliana kwa ukamilivu, watakata shauri ikiwa yastahili gharama au ile faida ambayo tutaipata, yastahili kulipiwa na treasury yetu.

Pia katika kazi, tumeulizwa hii national council kazi yakeitakuwa nini? Kazi yake itakuwa sawa sawa na national assembly. Kazi ambayo ya national assembly ni kazi tunaijuwa ya Bunge. Kutizama mizania ile au budget ya nchi, kufanya uchunguzi katika budget na mali ya Serikali inatumiwa vipi, kuweka sheria au kutengeneza sheria, siyo? Basi hiyo national council itafanya kazi hiyo hiyo, yaani ile bill, au ule mswada wa kanuni, waweza kutoka pande zote mbili. Mtu anaweza kuanzisha bill kutoka national council. Ikisha, national council ikisha pitisha, inapelekwa national assembly nafikiri. Au itatoka national assembly kwenda national council and vice versa.

Pia tumegawanya kazi za hizi sehemu mbili za Bunge au nyumba hizi mbili za Bunge. National Council kwa mfano, ndio ambayo itatoa .....(Inaudible). Itakubali watu kuwekwa katika commissions au Tume muhimu sana ambazo tumezifikiria kwamba zitatusaidia katika nchi yetu.

Judiciary Service Commission: Ile commission ambayo kazi yake ni ku kodisha, kuwapatia kazi ma-judge na kadhalika. Members wa hiyo commission lazima members wa national council wasikubali au wakubali. Ile list lazima ikubaliwwe na iwe approved by the National Council.

Pia Ethics and Integrity Commission: Wana chama kwenye hii commission pia, lazima wakubaliwe na National Council. Na hii ni commission mpya, tunafikiria kufanya. Ethics and integrity. Hii commission ni muhimu sana. Hii ndio commission ambayo

itachungulia mambo .....(Inaudible) ya ufisadi nchini. Na kuchungulia kila mtu ambaye amefanya makosa na kukata shauri huyu amefanya makosa na lazima afanyiwe nini. Na ambayo itahimiza watu kuishi na kufanya kazi zao za kiserikali kwa njia inayo faa. Na kuwatambuwa wale ambao hawafanyi kazi vizuri. Ethics na integrity, integrity ni mtu ambaye ni honest. Mtu ni mwaminifu na kadhalika. Ethics inakaribiana na dini kwa hakika, inahusika na dini. Kwa hivyo commission itakuwa kazi yake ni kuhakikisha kwamba wafanyi kazi wa Serikali na wote ambao wanafanya kazi ya uma na wananchi wanafanya kazi yao sawa sawa. Na yule ambaye hafanyi kazi sawa sawa wampatie njia ya kutiwa adabu.

National Land Commission pia, wana chama wa land commission hii lazima wakubaliwe na national council.

Teachers Service Commission: Salaries and Remuneration Commission, commission hii, tume hiyo inahasika na mishahara ya wafanyi kazi wote wa raia. Tangu Rais mpaka messenger, mishahara yake itakatiwa shauri na salaries na remuneration commission. Constitution Commission. Tunasema kwamba, hii Constitution tukisha maliza kazi zetu, wapatie wenzetu watano hivyo sita, ambao kwa muda wa miaka miwili mitatu hivi, watahakikisha kwamba yale yaliyomo hapa, au yale yaliyomo katika Katiba mpya, yanafuatwa, yanatekelezwa.

Commission on human rights and administrative justice. Hii pia ni commission mpya ambayo tumependekeza ifanywe. Human rights, haki za binadamu, itakuwa inachungulia haki za kila raia kwamba haki za binadamu, na katika members wa hii commission, atakuweko yule Ombudsman, public protector. Katika kuzunguka kutoa maoni ya wananchi, tumeambiwa na wananchi kadha, kila eneo la Kenya, tuweke Ombudsman. Neno hili latokana na kule pande za Sweden au Scandinavia. Huyu ni mtu ambaye ofisi yake, si yeye mwenyewe peke yake, lakini ana ofisi, na watu wake ambao wanachunguwa malalamiko ya raia wa hada na yeyote kati yetu. Ana taabu taabu na mashaka, anakwenda katika ofisi hii ya Ombudsman, anaeleza shida zake. Ofisi hiyo ina haki na wajib wa kufanya uchunguzi katika malalamiko yale kuhakikisha kwamba ikiwa ni sawa au si sawa. Na kujadili, na kujaribu kumsaidia yule mwananchi ikiwa ana malalamiko. Basi huyo, tunamuita public protector sisi, badala ya Ombudsman. Huyu basi atakuwa katika hii Tume. Inahusika na human rights and administrative justice.

Na director of Public Prosecution, Public Defender, Police Commissioner pia Mahakimu na Chief Kadhi. Wote hawa majina yao lazima ya kubaliwe National Council.

Pia kwa upande wake National Assembly tumewapa kazi zao. Wao wataa-approve Prime Minister, jina lake, wata-approve Deputy Prime Minister, Waziri, Waziri mdogo, Permanent Secretary, Balozi au High Commissioners, Electoral Commission, members zake, ndio hii commission members, wake Auditor General, Controller of Budget, Director of Central Bureau Statistics, na Governor wa Central bank. Wote hawa lazima national assembly ikubali. Wakichaguliwa na rais, wakubaliwe na national Assembly, na kadhalika. Hizo ndizo kazi za nyumba hizi mbili za Parliament mpya.

Nafikiri yale mengine ni kama desturi, pia kura zitahesabiwa pale kwenye ile polling station sasa. Hazichukuliwi pale kwingine.

Na zitahesabiwa pale pale, ikiwa hapa ni kituo cha kupiga kura basi mwisho wa kupigwa kura basi zitabaki hapa kura zitahesabiwa.

Pia boxes zile, sanduku za kupiga zitakuwa transparent, wazi, unaweza kuona ndani. Mambo kama haya ndiyo mabadiliko ambayo tumefanya.

Kisha tunaendelea katika sura ya sita, ambapo tunazungumzia the Executive. Executive, Serikali ina sehemu tatu, kuna sehemu ya Executive, kuna sehemu ya Judiciary na legislature. Legislature tusha maliza, siyo? Executive ni rais na cabinet, na baraza la mawaziri na civil service. Hawa ndio Executive, hawa ambao baada ya sheria kutolewa ndio wanahakikisha ya kwamba kazi itafanyika kufuatia ile sheria.

Na tunazungumzia mambo ya kazi za Rais, nani anaweza kuwa Rais, nani ana-qualify kuwa Rais na kadhalika. Rais tumezungumza na kazi zake kwamba, yeye ndiye atakaye funguwa Parliament, yeye ndiye ambaye anaweza kuita Parliament kukutana tena akitaka kusema nao, yeye ambaye ata i-dissolve Parliament, lakini kufuatia Consitution. Na Constitution tunasema kwamba, Parliament itakuwa dissolved katika hali fulani, si wakati wowote. Tunasema kwa mfano kwamba, Rais ndiye atakaye mchaguwa Waziri mkuu. Kutakuwa na waziri mkuu na mawaziri, atawachaguwa rais lakini lazima national assembly iwakubali, okay. Lakini katika, na atakaye chaguliwa kuwa ni waziri mkuu na yule mkuu wa chama kilicho pata majority katika Parliament, sawa, kama ilivyo katika .....(Inaudible). Lakini huenda kuwe na Waziri Mkuu asikubaliwe na, lazima akubaliwe na Parliament. Wamkubali huyu kuwa ni waziri mkuu. Wakimkubali ataendelea na kazi yake. Kisha yeye waziri mkuu atawachaguwa mawaziri wake, lakini mawaziri wote watachaguliwa kutoka nje ya Parliament. Watakuwa a non-MPs. Waziri mkuu mwenyewe ni MP maanake atakuwa ni mtu, Member of Parliament na leader of the majority party, lakini waziri wake watatoka nje. Sasa Parliament lazima iwakubali wote wale, wanajuwa huyu Waziri Mkuu na hao mawaziri wake.

Pia mawaziri wadogo, ikiwa ni rais amchaguwa huyo kiongozi wa chama kilich opata viti vingi zaidi katika Parliament. Ikiwa Parliament haitamkubali yule, na Serikali yake, Rais lazima amchaguwe mwingine. Ikiwa huyu mwingine huyu pia hata kubaliwa na Parliament, lazima sasa, Rais ai-dissolve Parliament, na ufanywe uchaguzi mwingine. Na tujaribu tena kuunda Serikali. Hayo ndio mabadiliko tuliyo yafanya. Lakini itakuwa ni jambo la nadra kabisa kuwa mambo hayo yatatokea. Lakini tumesema kwamba, ikitokea hivi ndivyo mtakavyo fanya.

Na pia tumesema kwamba, kutakuwa pia na Deputy Prime Ministers wawili. Hawa deputy prime ministers pia watakuwa ni wabunge. Prime Minister na Deputy Prime Ministers ni Wabunge.

Mawaziri, watakuwa si wabunge. Hayo ndio mabadiliko tulio leta. Kwa hivyo Rais anaweza kuvunja Bunge katika hali kama hizo ambazo nimezitaja. Rais ata-appoint au atachaguwa cabinet, baraza la mawaziri kama nilivyo eleza: Mkuu wa Waziri au

Waziri Mkuu, Deputy Prime Minister, waziri, makamu wawili wa Waziri Mkuu, na si zaidi ya mawaziri wa kumi na tano. Tumesema kwamba, waziri wawe kumi na tano tu. Na manaibu wa mawaziri kumi na tano. Lakini jana tumesikia kwamba watu walisema kwamba tuongeze iwe twenty. Lakini kama nimesema, haya ni mapendekezo, yote haya niliyo yasema, ni mapendekezo tu. Mabadiliko ambayo tunafikiri kwamba ni vizuri kufanyika. Lakini sasa itategemea national conference, pale ndipo patakapo katwa shauri.

Ukitaka kuongeza idadi ya mawaziri watoengeza. Ikiwa itasema la, hutuwezi gharama ya kuwa na majumba mawili ya Parliament kwa sababu tutaendelea na nyumba moja, National Assembly na kadhalika.

Pia tunasema kwamba, with prior consent of the cabinet, the President may appoint commissions of enquiry, tume za uchunguzi, yataweza kunino. Pia hata, baada kushauriana na baraza la mawaziri na national defence council, au baraza la ulinzi wa taifa, Rais aweze ku-declare state of emergency, hali ya hatari nchini na kadhalika.

Kazi kama hizo ndizo atakuwa nazo Rais, na si kazi ndogo, yeye pia atakuwa ni symbol of unity. Jambo hili ni muhimu sana. Ndio atakuwa ishara ya umoja wa nchi, Rais ana heshima yake kubwa. Ishara, yeye pia atakuwa head of state. Inaitwa dola. Atakuwa commander-in-Chief of the Defence Forces, Mkuu wa majeshi. Atakuwa chairperson of the national security council. Baraza la amani ya nchi. Pia Chairman of the Defence Council. Baraza la ulinzi wa nchi. Kuna baraza mbili hapa. Na pia atakuwa kama nilivyosema symbol of unity of the nation na jukumu la ku-promote, la kuendeleza, na kusitawisha umoja wa nchi.

Pia kuhifadhi ufalme wa nchi. Sovereignty of the nation. Hiyo ni kazi yake Rais na pia tu-promote and respect for the diversity of the people. Kuhakikisha kwamba kuna heshima kwa kila sehemu ya uraia wa Kenya. Kabila zote, dini zote na kadhalika. To uphold, safeguard, and respect the Constitution. Atalinda Katiba, ya nchi na kadhalika.

Kisha tunatoa qualifications zake, awe nani, nani aweza kuwa Rais. Lazima awe kama citizen of Kenya, raia wa Kenya kwa kuzaliwa, awe ni kati ya miaka thelathini na tano na sabini. Isiwe zaidi ya sabini, au siyo chini ya miaka thelathini na tano. Kuna baadhi ya wananchi kwa sababu hawa young people wasema kwa nini hampunguzi zaidi, sisi pia tuna ambition. Tuna tamaa ya kuwa Rais. Lakini tumeona kwamba 35 ni umri ambao ni wa mtu mzima amekuwa mziwa amekomaa kwa kutosha. Amekomaa si sana lakini kwa kutosha.

Sabini, pia ni muhimu kusema kwamba, sabini ni kwa elections, baada ya hii elections itakayo sasa. Kanuni hii ikipitishwa, haita husikana na elections za zitakazo kuja hizo. Kwa hivyo wale ambao wanazunguka na kusema kwamba tumesema hivi ni kwamba Kibaki asisimame because he is over 70, au jamaa wengine la si hivyo: Elections hizi za kwanza zitakazo fanyika, itakuwa hakuna kiwango cha umri .....(Inaudible).

Pia awe na degree ya chuo kikuu. Lazima awe degree holder na pia tumesema kwamba asiwe Mbunge. Na akisha kuwa Rais

asiwe na uhusiano wowote na chama chochote cha kisiasa, hivi ni kuhakisha kwamba atakuwa neutral. Hapendelei chama hiki au chama kile. Hana uhusaino na chama chochote. Hayo ndio mambo muhimu yalioko katika mswada wa Katiba. Na atakuwa na terms mbili tu. Pia wabunge na term mbili tu. Maximum, zaidi kabisa ni miaka kumi. Ataingia, atakaa miaka mitano. Atajipeleka mbele pia kwa uchaguzi utakaofuata, akifaulu, ataingia, lakini baada ya hapo, atakaa kando huyu jamaa mwingine apate nafasi kuingia.

Kisha tunaingilia ile sehemu ya tatu ya Serikali. Judiciary and legislative system. Na hapa tumeweka korti mpya, mahakama mpya, supreme council, supreme court ambayo haikuweco hapo awali. Yaani juu ya high court, court of appeal, tumeweka juu zaidi supreme court, supreme court itahusika na mambo mengi sana kwa mfano kukiwa jambo linalohusu Katiba, supreme court itafikiria hayo mambo ya Katiba. Court of appeal haihusiki, na kisha kuna subordinate courts. Court ndogo na hapa kuna magistrate courts na pia kadhi's court, mahakama ya kadhi.

Na hapa tumefanya mabadiliko fulani katika mahakama ya kadhi, tumesema kwamba kuweco na ikiwa ni idadi ndogo kabisa, kadhi's courts kuna tatu kwa sasa ndio ziweze kuzidishwa baadaye. Na tunasema kwamba mtu ikiwa hakustosheka, na uamuzi wa kadhi anaendelea na senior courts, provincial courts, na pia hapo aende kwenye court of appeal. Na court of appeal atakuwemo chief kadhi na wenzake wawili. Makadhi pia, hivi ni kuhakikisha kwamba jambo lolote la mhusu mwisilamu kwa upande wa talaka, kwa upande wa kuoa, kwa upande wirathi, inazingatiwa na itaamuliwa na waisilamu, ma-judge wa kiislamu kabisa.

Appeal pia itakwenda kwa waislamu. Itakwenda supreme courts, hii ni katika hali moja tu, ikiwa kutakuwa na mabishano. ....(Inaudible) katika court of appeal, mmoja katika wawili ambao wemegombana, hakustosheka na court of appeal, kufuatia taksiri ya sheria ya kiislamu. Kwa hivyo inaeza kwenda supreme courts. Lakini kule supreme courts atakuweco pia na chief kadhi, na hapo mazungumzo na majadaliano itakuwa kuhusu na, kuhusu ile sheria ya kiislamu yenyewe. Hawata fuata sheria yoyote ile.

Pia tumesema kwamba kutafuatwa procedure, ambayo itaundwa sasa hivi kiupya. Maana yake hivi sasa tunafuata procedure ambayo haina msingi, si ya sawa kabisa katika korti za kadhi. Kwa hivyo atakaa chief kadhi na wana sheria wengine ambao wana maarifa ya dini ya kiislamu, kuweco ile njia kuchungulia kesi yeyote. Maana zile procedures, mnamia procedure ambayo si ya kiislamu. Na kwa hivyo chief kadhi ata kaa na hawo wenzake, chief kadhi chairing consultation of the chief justice, and the law society of Kenya make rules of courts for the practice and procedure to be followed by the kadhi's courts. Wanataka mambo inaendeshwa ovyo ovyo tu, ukiingia kwenye korti ya kadhi utaona kwamba, jinsi ya kufungua ile kesi, jinsi ya kufuata haina mwenendo wake, haiana system yake. Lazima system iweko kama vile iko katika korti nyingine vile. Ili kwamba tupate korti za kadhi ambaye anafuata mwenendo kwa kirasmi katika kuchungulia jambo lolote la kadhi.

Pia tunasema kwamba the chief kadhi shall have the same status, privileges and immunities as the high court judge. Atakuwa na

sawa sawa na high court judge. Na pia senior kadhi atakuwa kama chief magistrate na kadhi atakuwa kama district magistrate. Usawa katika mshahara, usawa katika zile privileges, mambo ya housing, makao na kadhalika. Kama kadhi hivi sasa ma kadhi wetu hawana, hawapewi heshima ambayo zaidi kwa kadhi. Na chief kadhi ndiye kabisa. Kwa hivyo mambo hayo lazima yabadilike.

Lakini pia, tumesema kwamba hawa lazima wawe na qualifications zao. Chief kadhi must be a muslim of not less than 35 years of age. Asiwe mdogo kuliko miaka thelathini na tano. Awe ni advocate of the high court, okay, kwa hivyo ni mwana sheria kwa korti zetu. Kama hawa wenzake wote wana sheria wengine kama nchi yetu, na iwe ana experience ya miaka kumi katika kazi hii ya kuwa mwana sheria. Na wale wenzake wengine kadhi na senior kadhi watakuwa pia advocates, wana sheria, ana qualification, qualification yake iwe muslim personal law. Amesoma sheria inayohusu muislamu na ambayo haija mwathiri katika maisha yake. Hawa watakuwa na experience ya miaka mitano tu yatosha, kadhi na , na kadhi baadaye atakuwa ni pia senior kadhi.

Judiciary service commission tuliitaja hapo awali, kadhi atakuwa ni member, kuakilisha service commission.

Jambo gani lingine ambalo linatahitajika hapa, mhimu kwa akina mama wa kislamu. A muslim woman will be also a member of judicial service commission. A muslim woman to represent the muslim community, nominated by the national muslim organization. Kutakuwa na, lakini pia huwa wana qualifications, ana maarifa ya kisheria na kadhalika.

Pia tumependekeza kwamba kila ofisi ya kadhi kuweko na mama mmoja ambaye ana maarifa ya sheria ya kiislamu, kumsaidia mama wa kiislamu akija, aona haya kuzungumza mbele ya kadhi na wanaume, amsaidie kueleza yale ambayo yatakayo kueleza bila kuona haya. Kwa njia hii atapata haki yake ipasavyo.

Nafikiri ni hayo ambayo nitakusema hapa, kwa upande huu, na sasa tutakwenda katika sehemu nyingine ambayo ni mhimu, chapter ten, hapo ni devolution of power, mgawanyo wa mamlaka. Katika kuzungumza, kuzungumza na wananchi hapa na pale, saa zile tuazunguka, nchini, tumeambiwa na watu wengi sana kwamba mamlaka alizonazo

Rais hivi sasa ni nyingi sana, lazima zipunguzwe.

Pia kuna wale wanao lalamika, kwamba raia wa wada ahisi kwamba yuko karibu na huduma au utumishi wa Serikali. Wengine wanasema sisi lazima tutoke hapo kuenda kule Nairobi kufuatia jambo ndogo kama title deed na mambo kama hayo. Kwa hivyo tumeona kwamba lazima tugawanye mamlaka kufikia mwananchi karibu zaidi. Hii ndio inaitwa devolution of powers. To devolve is to spread out, kutia chini zaidi ifike mbali zaidi. Kwa hivyo, lengo la kufanya hivyo, ni kuleta serikali na soma hapa, lengo la kufanya hivyo ni kuleta Serikali na kila aina ya utumishi wa Serikali, na taasisi zake, na idara zake; karibu zaidi na mwananchi.

Pili, kustawisha zaidi maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kumfikia kila mwananchi na kufikia kila sehemu ya nchi. Wananchi wamekuwa wakisema kwamba upande wetu hapa hatuna bara bara, tuna mazao lakini hatuwezi kuzipeleka sokoni maana bara bara ni mbaya, tukipata ugonjwa hatuwezi kufika hospitali, hii bara bara ni mbaya na kadhalika.

Tatu, kuhakikisha ya kwamba mali za asali za nchi zinagawanyika kwa uadilifu zaidi. Nchi na mali, mali inangia kutoka kwenye kodi na njia nyingine, kuna mali kutoka mali ya asili, kutoka mwitu, kutoka bahari kutoka national park, na kadhalika. Kwa hivyo watu wanasema kwamba tuhakikishe kwamba mali za hasili zinagawanyika kwa uadilifu zaidi. Pande za Taita Taveta tunajuwa kwamba kule kwetu, hapa kwetu wanyama ni ghali zaidi na wanadhamana zaidi kuliko sisi raia. Kwanza wanafikiria ya wanyama kuliko sisi. Watalii wanakuja hapa kwetu kutizama wanyama, mapato inapatikana, hatuoni chochote, hali yetu iko chini zaidi kuliko hali ya wanyama. Kwa hivyo lengo la kufanya mgawanyo wa mamlaka ni kuleta faida ya mali ya kiasili kufikia kila eneo la nchi.

Nne, kugawanya mamlaka ya Serikali kutoka Serikali ya kati, central Government kufikia mashinani. Kwa hivyo tumependekeza kuwe na serikali ya kijiji. Kila kijiji kitakuwa na baraza lake. Wazee wa kijiji watakutana pamoja kuzungumzia hali ya kijiji chao. Na kupandia juu tunasikia location council. Baraza la location, na baraza hili litachakuwa wajumbe wawili kutoka kila kijiji. Na watazungumzia hali ya sasa location yao. Kwanza kijiji, kisha location.

Kisha kutakuwa na Serikali ya wilaya, district council or district Government. Baraza la, hapa kutakuwa na uchaguzi haswa, kule jamaa wata katika, vijiji, wanajulikana wazee wa pale, lakini hapa katika district, ndipo ambapo kutakuwa na mamlaka ya haswa. Kutakuwa na elections, kutakuwa na district council, na district council ndio inaweza kuwafikiria hali ya district nzima kwa kila eneo.

Na kutakuwa na mamlaka kupawa hii district council na wana chama wa district council kama nilivyosema watachaguliwa kwa kura za wananchi na idadi yao itakuwa kati ya ishirini na thelathini kwa kila district. Baraza la wilaya la watu kati ya ishirini na thelathini. Juu ya hapo kutakuwa na provincial Government na provincial council. Kweli district council itasimamiwa na district administrator not district commissioner, district administrator. Haihusikani kabisa, na utawala ulioko hivi sasa maana hawa ni, wamechaguliwa na wananchi. It is an elected district government and run by the district itself. Na itakuwa na powers zake ambazo zitaja hivi sasa.

Kisha kutakuwa na provincial, Serikali ya mkoa, na huko kutakuwa na provincial administrator. Hapo pia, hao watakuwa tu waakilishi wawili kutoka kila district katika mkoa, wataingia katika hiyo provincial council na watasimamiwa na provincial administrator. Kazi ya provincial council itakuwa ni kuzungumzia hali na mahitaji ya wilaya zote katika ile province. Kushauriana na, maanake hawa watakuwa ni wajumbe, two from each district, watazungumzia na kushauriana juu ya kusaidiana. Kwa mfano district council ya Malindi na Mombasa watakutana kule kule na wa Lamu na wa Kwale na kadhalika, na Kilifi watakutana pamoja. Watazungumza juu ya hali ya ustawi wa provinces lakini nguvu zitakuwa kwenye district. Wale ni

kushauriana tu.

Na pia, inawezakana kuwa district mbili, kushauriana, kusaidiana katika kustawisha eneo lao. Mombasa na Malindi, Kwale na Mombasa, Lamu na Tana River na Kadhalika. Kufikiria hali yao pale, na wana hitajia bara bara wanahitajia clinic hapa na pale, tufanye hivyo.

Na Serikali ya kati, itakuwa na waziri maalum kufanya mashauriano na councils hizo, na kufikiria mahitaji yao. Na Serikali ya kati itakuwa ikiipa kila district au kila sehemu msada wa kipesa ikihitajika. Mara kuna district zingine ambazo ni tajiri. Ingingine ni maskini, ingine wastani, kwa hivyo yule ambaye ana hali yake au district ambayo hali yake iko mbaya sana, itasaidiwa kwa pesa kutoka central Government.

System hii, ya mpango huu tulifikiria kuliko mpango ule wa majimbo .....(Inaudible). Maanake hapa. Serikali itakuwa iko karibu zaidi kwa mwananchi kuliko provincial au regional. District ndiyo itakayo kuwa na power. Na hapa, ningependa kueleza juu ya mamlaka ya district council, page 45.

Na national Government, Serikali ya kati, itahusika na ulinzi kama, ulinzi wa nchi nzima, utahusika na international relations, mambo ya mahusiano na nchi za kigeni, telecommunication, mawasiliano ya kila aina, national resources, mali ya asili ya nchi, treasury kule, national elections, formulation of national policies siasa ya nchi nzima kuhakikisha kwamba currency, pesa, court, mahakama, .....(Inaudible) citizenship, immigration, national public service, control and management of disaster, maafa, central bank, na mambo kama haya.

District, Local taxes, kukusanya kodi, education services, huduma za elimu ya kila ustawi, elimu ya nursery, primary na secondary.

Medical na health services, utumishi wa matumishi wa matibabu. Water services, ya maji, road services, itakuwa kwa kila district itashughulikia pia mabara bara yaliyoko katika ile district na kodi yake pia itatumiwa pale pale, juu ya kusaidiwa na central government, kutoka natural resources.

Market and trading centers. Kisha kutakuwa a district planning, hawatakuwa na orders from Nairobi. Pale pale ni district ita-plan yenyewe jinsi ya kueneza bara bara, jinsi ya kueneza mawasiliano, stima na kadhalika.

Agricultural services, zitakuwa local, huduma za kilimo na kadhalika. Land survey, land administration, trade licences, cooperative development, social rehabilitation, labour matters, mambo ya wafanya kazi na kadhalika. Human resource, management and development, inahusika pia na kazi na jinsi ya kutumia wananchi katika kazi tofauti.

Community development, council .....(Inaudible) na kadhalika maana at the district level, ile district itakuwa na hamu zaidi



kuyaeneza, kustawisha mambo ya kitamaduni maana ni ya pale, ya pale pale, sawa? \$ *End of tape two side A*

Mamlaka ni, itakuwa ni tofauti kabisa, lakini nimesema hayo ni mapendekezo. Tuone jinsi ambavyo conference ita, national conference itafikiria jambo kama hili. Mwisho kabisa nafikiri kabla ku, kabla ya kumaliza tupate maoni yenu, tatazungumzia mambo ya ardhi. Jambo hili la ardhi, pia mhimu sana, tumelifikiria sana lakini tukagereki kwamba kuna Tume nyingine ya Njonjo ambayo kwa njia ya mahsus kabisa ilishikilia jambo kama hili la land na report yao bado kutolewa. Hatujui yaliyomo, ni confidential, na sisi ikawa kidogo tumesema kwamba hatutaki tujaribu tuseme neno ambalo litakuwa baadaye litagongana na pendekezo lolote katika Njonjo commission wakati alipo.....(Inaudible). Lakini tumesema haya, kuwa katika muda wa miaka miwili, baada ya Katiba hii kukubaliwa, kwa rasmi, Bunge itapitisha sheria na kuweka kanuni zinazohusu ardhi na kuweka taasisi na siasa kushuluhisha kila ugomvi unao husu ardhi na mashamba kwa njia inayofaa. Mara tumesikia mengi, malalamiko mengi tukasema kwamba kwa kuwa hivi sasa kuna kanuni nyingi sana kuhusu ardhi. Kwa hivyo kuna haja ya Serikali kukaa kwa makini na wakati huo utakuwa ushapata Njonjo commission. Kuweka kanuni zote zinazohusu kwa njia inayofaa, na kwa njia ambayo itasuluhisha au kuondoa matatizo yaliyoko katika eneo hili tangu hivi sasa.

Pili tumesema kwamba katika muda huo huo wa miaka miwili wale wanaoitwa ma-squartter, wale ambao hawana ardhi, hawana makao, wanasumbuka, mara waanambiwa waondoke na kadhalika, swala hili la u-squartter na landless liondolewe katika nchi, wapatiwe makao katika muda wa miaka miwili.

Pia tunasema kwamba katika muda huo huo pia, kufanywe uchunguzi katika mashamba na ardhi zilizotolewa hapo awali. Tumepata malalamiko ardhi zetu zilichukuliwa hapa na pale, kwa njia isiyo haki. Kuna haja kwa hivyo kufanya uchunguzi katika mashamba na ardhi zilizotolewa na Serikali ili kuhakikisha ikiwa zimetolewa kwa njia ya sheria au la, ikiwa imetolewa kwa njia ya sheria basi, zirudishwe katika mikono ya serikali.

Na nne, katika muda huo huo wa miaka miwili, lazima kupatikane njia za kuchungua na kupata mahasio ya malalamiko kuhusu ardhi ya watu wa Pwani, watu katika zile mashariki na Rift Valley. Hapa kuna matatizo makubwa .....(Inaudible). Na pia kwingine ambako ili kujuwa ikiwa malalamiko ya watu hao yana msingi au la. Na yakiwa msingi pia yata .....(Inaudible). Haya ndio mapendekezo yetu kuhusu ardhi na mamlaka mengine.

Nafikiri nitakoma hapa ili kupata maoni yenu. Samahani nimechukuwa muda mrefu lakini yalikuwa ni mambo ambayo ni muhimu kuyaeleza kwa kuwa wengi wenu hawana nakala yoyote ya huu mswada wa Katiba, kwa hivyo ilikuwa ni muhimu. Lakini kuna mengine, kuna sura nyingine lakini hayo kwa kuwa wakati hatuna, tutazidi musome wenyewe kisha mtupe maoni. Kama nilivyosema, lengo la kuja hapa leo, ni kuwaelemisha juu ya hii Katiba ilivyo, yaliyomo, na ni hatua gani ambayo itachukuliwa. Baada ya sasa kwamba tukisha maliza hapa, tutarudi Nairobi, tutafanya huo mkutano mkubwa, waakilishi wenu na Wajumbe Wabunge, wawakilishi watatu kutoka kila district kama nilivyosema, wajumbe kutoka, waakilishi wa kidini, akina mama,

walemavu na wafanyi kazi na kadhalika, wote watakutana, watazungumzia, hiyo ndiyo hatua watakayo ifwata na baada ya hapo, tutabadilisha tena Katiba kufwatia mapendekezo ya National Conference. Na tukiibadilisha kufuatia mapendekezo, not mapendekezo tu ya national conference lakini, maagizio yake. Badilisheni hizi, badilisheni zile, ondoeni hili, tieni hili, tutabadilisha kufuatia amari ya conference, ipelekwa bungeni iwe ndio Katiba yetu. Shukrani sana, *Asalaam aleykum..*

Sasa tutapokea maswala na pia mtu akiwa na maneno la kusema. Pia tunasema ikiwa kuna haja ya kuandika lolote, tutapokea pia maoni yako ya kuandikwa, ndio ya maktaba. Nitampa kila mtu number yake, kisha nitawaita mmoja baada ya mmoja. Number one, nani mwingine? Number two, number three, number four, number five. Tafadhali kumbuka number yako. Number six, number six, number seven, number eight, number nine, number ten. Nitachukuwa hawo kumi kwanza. Mweze kuzungumza, na utaandika .....(Inaudible). Majina yako tafadhali.

**Mr. Mohammed Farah Abdi:** Mimi majina yangu kamili ni Mohammed Farah Abdi.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Mr. Mohammed Farah Abdi:** Mohammed Farah Abdi. Kwanza nilifurahi kidogo kusikia kwamba kulingana na aidha, kwamba kutakuwa na kamati ya Serikali, itakuwa inashughulika na mambo ya pay, maana mambo ya pay kama kuhusiana na mshahara. Maanake, katika sheria ya Kenya, mimi nimewahi kufanya katika jeshi la Kenya hapa kwa miaka ishirini na nne. Kuanzia nikiwa askari, mpaka nilikofika warrant officer, na kutoka hapa nakaendesha Kenya ferry. Maanake mshahara huongezwa na pay review, wala si mtu kujiongezea. Imekuwa ni kawaida Bunge kujiongezea mshahara, siku moja tu wakajadiliana, na wakaongeza hiyo mshahara vile wanapofikiria, na wakapitisha. Na hiyo, hata mimi nilifanya hivyo, ukiniambia jiongezee mshahara, nitajiongezea, mpaka ifike milioni moja. Maanake si sheria kabisa mtu kupewa nafasi ya kujiongezea mshahara.

Ya pili, mimi nilipoingia katika jeshi la Kenya, jeshi la Kenya huwa linafanya screening kwamba hakuna mwananchi ambaye ni wakutoka nje ataajiriwa katika jeshi la Kenya. Lakini kulikuja kutokea wakatim fulani, jamii ya Wakristo hawakutoa kisomali, wote walifanyiwa screening hapa Kenya, isipokuwa, wale walipokuwa katika jeshi, kwa sababu wale walikuwa katika jeshi tayari walifanyiwa screening kabla hawajaingia katika jeshi. Sasa, tulipoacha jeshi, tulipata kitambulisho kiingine mpya, mmoja wao ni mimi? Kitambulisho changu kikapotea, na kwa vile siku ile nikifanyiwa screening, watu wa jeshi walikuwa exempted, sasa nimekatanzwa kitambulisho maanake sina screening card. Na kama siyo ati, kwanza kwa vile nilipotoka ferry mimi nilienda United Arab Emirates, nina passport, basi nikikuonyesha singeweza kupiga kura. Kwa hivyo kuna tatizo ya kwamba, jamii, wale ambao wanatoka North Eastern wengi, wale walipoteza kitambulisho, nafikiri ni card zilikuwa zote, zilitolewa mara moja tu, na wengi walipoteza, wengine mtu akaoshea ndani ya nguo. Wengi hatapiga kura, maanake hawana kitambulisho wala

hawaruhusiwi kupewe kitambulisho without that screening card. Thank you very much.

**Com. Prof. Salim:** Na ulieleza mambo hayo, wakaambiwa nini?

**Mr. Mohammed Farah Abdi:** Walisema mpaka uje na screening card. Na mimi nikawaambia wale tulipokuwa tukipiga jeshi, tuliambiwa hatuwezi kuwa screened kwa sababu nyinyi mumekuwa screened kabla hamjaingia jeshi.

**Com. Prof. Salim:** Hivi karibuni tumeweza kufanya .....(Inaudible).

**Mr. Mohammed Farah Abdi:** Walisema hivyo, lakini nilipoenda Nairobi, walisema hiyo ilikuwa ni kwa maneno tu, it was just verbal and then I have got a written.

**Com. Prof. Salim:** .....(Inaudible).

**Mr. Mohammed Farah Abdi:** Ni jambo ambalo linapaswa lifuatwe.

**Com. Prof. Salim:** Number two, .....(Inaudible). Number two utasema jina.

**Speaker:** Number two.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Mr. Sirahi Mstafa:** Kwa majina naitwa Sirahi Mstafa kwangu mimi mada yangu hapa ilikuwa ni kuhusiana na hii national conference. Nimesema kuwa hayo mapendekezo yenu, kama mlivyo yatoa kwa raia, yanakwenda moja kwa moja mpaka Nairobi kwa national conference, yajadiliwe, tujue tuta-delete gani tu-insert gani, and then to insert journey. Wasiwasi wangu nikuwa, hiyo picking, ya hao delegates how fair was it? To wa-entrust na huo uwezo wa .....(Inaudible) kitu katika hiyo .....(Inaudible) ambayo inatengenezwa na wananchi.

Jambo la pili, nikigusia hapo hapo katika hao Wajumbe waliokwenda kule, maybe, unajuwa the whole process, vienye imeendelea, imekuja mpaka imekuwa .....(Inaudible) bado kidogo kila mtu anavutia kwake. Huyu mwingine anavutia kule, mwingine anavutia huku. Sasa shida yangu ni kwamba, wale ma-delegates ambao wamepelekwa kule katika national

conference, ikiwa tutawapa huo uwezo kuwa wakiwa direct kuwa hili ondoweni, hili mliweke na hili muondoe ili mlieke. Huenda ikawa wale ma-delegates, majina yao yamechukuliwa kimpangilio, kusudi waende wafaye aidha jamii fulani, ama kundi fulani la kisiasa. Kwa hivyo kwa maoni yangu nilikuwa naona haki hiyo kwanza, kufaa kupewe kuwa wataondoa jambo hili waseme tuweke, labda ukinjibu baadaye, huyo utaratibu ndio tuliotumia kuwachaguwa, mpaka wakuambie hili utaeka hili usiweke. Labda utanielezea baadaye utaratibu huwo kama .....(Inaudible).

Jambo la pili nini,

**Com. Prof. Salim:** La tatu.

**Mr. Sirahi Mstafa:** Jambo la tatu, umesema majukumu ya national Government na local ama district? Umeguzia kitu registration of people or person kama ninavyo waambia katika hali. Kitu sielewi ilikuwa, tunavyozungumzia kuwa registrations of persons zitafanywa na national Government, hiyo ina maanisha kuwa bado process hii itatupeleka kule kule Nairobi ama tutafanya nini yako hapa, watakuwa na hizi process hapa hapa karibu?

Jambo la pili, kuna neno kama driving licence.

**Com. Prof. Salim:** La nne.

**Mr. Sirahi Mstafa:** La nne, kidogo, malalamiko yangu ni mbili, sasa wewe, uko pale pale. Kuhusiana na hiyo hiyo registration, kuna vitu kama driving licence, kununua vitu kama passport, sijui kama vitakuwa kwa central Government ama vitakuwa kwa hii local yetu sasa? Na kama zitakuwa kwa central, yes, lazima tutaenda kuzipata Nairobi, ama zitatengenezwa hapa karibu kule tulipata. Asante.

**Com. Prof. Salim:** Number three,

**Mr. Hamisi Mwinyi:** *Salaam Aleykum.* Prof. Ghai, wananchi watukufu, ah, Prof. Salim, kwanza ningetaka kushukuru Tume ya

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Mr. Hamisi Mwinyi:** Ningependa kushukuru Tume ya,

**Com. Prof. Salim:** Majina?

**Mr. Hamisi Mwinyi:** Kwa jina naitwa Mwinyi Hamisi Mwinyi, natoka Shika Adabu. Kwanza nataka kushukuru wananchi watukufu, kwa kukaa kimya, na kujituliza kwa muda wote huu mrefu, wakiwa na machungu pengine, unyanyasaji na ugandamizaji wa Katiba hii tuliyo nayo sasa.

Pili, ningeshukuru Tume ya kurekebisha Katiba kwa kazi yao nzuri sana, safi waliyofanya kwa muda mrefu ambao wengi wetu hatukutumaini kama wafikia lengo lao. Lakini leo, tunashukuru Katiba iko hapa, tunajadili, na baadaye itakwenda katika ngazi ya juu ikajadiliwe.

Pia ningeguzia kwamba, demokrasia ni kitu kinacho kuwa pole pole. Hata pengine Serikali kubwa kama zile Marekani au Uingereza ambao sisi tunasema in a demokrasia, pia bado kuna upungufu. Kuna upungufu mkubwa, ukisikiza ma-radio au kuona katika television, utaona pia hao wana lalamika, kwa hivyo kimepungua, hiki kimekamilika, hiki kina kasoro, mambo kama hayo. Kwa hivyo sisi hapa Kenya, ili tusizivunje moyo tukaona ah, hii Katiba yetu namna gani? Hii nafikiri imegusia maoni, hisia, na uoga, kila mtu na vitu hivyo vitakuwa addressed wakati mnapokuja jinsi tunavyo kwenda.

Bwana Idha amezungumzia maneno mengi hapa, mimi sitazungumzia sana. Lakini mimi kidogo ningetaka kuguzia swala la ardhi. Nafikiri swala la ardhi ni swala nyeti sana kote nchini, hasa hapa kwetu pwani. Tumekuwa tuna moyo mchungu sana, tumeteseka siku nyingi, swala la ardhi lilikuwa likimguza, kichwa na roho ya kila mtu. Nafikiri yote hayo, lakini ardhi, swala la ardhi linatoa kichwa juu. Sasa Bwana Idha amesema kuwa hawakuliguzia swala hilo. Limewekwa kati, limewekwa pembeni kodogo kwa sababu walingojea Tume ya Njonjo. Na ninavyo elewa mimi Tume ya Njonjo zimekuja siku, mara nyingi sana, zaidi ya tatu. Tume ya kwanza pengine ilikuja mimi sijaoa wala sijapata mjukuu. Lakini leo nina mjukuu, na bado Tume za Njonjo zinakuja.

Sasa namuuliza Bwana Idha, na pengine ningedokeza pia, hili swala la ardhi, wangeli zungumzia, wasingoje nini, kwa sababu hatujui kama hizo Tume, za mbeleni nazo tulizungumza jambo hili, zilifanyika Tume, lakini hatukujuwa matokea ya Tume hizo ilikuwa nini. Sasa hii nayo, ilichaguliwa nafikiri mwaka tisaini na tano au tisaini na sita, sijui ni mwaka gani. Lakini mpaka leo leo imekaa chini hivyo hivyo, haizungumzii, iliona nini, ikafanya nini. Sasa ilikuwa ni matumaini kama hiyo Tume ya Njonjo itawasiliana na hii Tume ya kurekebisha Katiba, wakae pamoja, wazungumzie swala hili. Kwa hivyo mimi, maoni yangu, na pengine maoni ya kila mwana Kenya, nahu Susan mwana Pwani, ni kutaka hili swala, wale national, wale delegates wakipelekwa, wasiliweke pembeni tena bali walichukuwe hili, iwe ni kitu hususan kizungumzia kwa wakati unao faa. Pinde tukipata hii Katiba, basi hili swala nalo liwe limetatuliwa, lakini, nafikiri. Waswahili walisema kungoja ngoja sana ni kuumiza matumbo bwana. Kwa hivyo, walai sina mengi ya kusema lakini mimi nilikuwa nataka kuulizia swala, asanteni.

**Com. Prof. Salim:** Nambari ya nne.

**Mr. Athumani Philip Ondasi:** Mheshimiwa Idaya, wazee mko hapa, *Salaam Aleykum.*

**Audience:** *Aleukum Msalaam.*

**Mr. Athumani Philip Ondasi:** Mimi kwa majina naitwa Athumani Philip Ondasi.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Mr. Athumani Philip Ondasi:** Mimi kwa majina naitwa Athumani Philip Ondasi,

**Speaker:** Endelea.

**Mr. Athumani Philip Ondasi:** Mheshimiwa, mimi kwa hakika, tumepokea maoni yako au mazungumzo yako, lakini kwa maoni yangu mimi haya kunipendeza hata moja, hata moja. Kitu cha kwanza, wakati mlikuwa Kizunguni kutoa maoni, na hakika hata mimi nilitamka, kitu tunaomba hapa Pwani, kitu cha kwanza ni majimbo, ndio itatuokoa unyanyasaji na maswali hiyo ingine yote tumeyapata miaka hii yote imepita. Hilo ni la kwanza.

Jambo la pili, nazungumzia hivi, hapa wewe umetuambia, Tume ya Njonjo sijui mngangoja ikafanye nini, ikafanye nini, nina hakika nyinyi, wewe na Tume yako, mliandikwa au mnasaidiwa na nguvu za wale watu mnao waona hapa ambao ndio raia wa Kenya. Hizo pesa au kitu chochote, gharama zote mlizotumia ni sisi. Kwa hivyo nyinyi, msinge jihusisha na Tume ya Njonjo, Tume ya Njonjo hatukuchaguwa sisi. Tume ya Njonjo anayo imani yule ambaye aliwachaguwa. Lakini sisi tuna imani na nyinyi mtusaidie, mtuondoe huu mzigo tulio nao kuanzia miaka iliopita mpaka saa hii. Raia wote tunao waona hapa kila mtu uweze kumwambia aende kwa benki akapate mkopo akitumia cheti cha ardhi, iko? Hakuna. Nimasikitiko mangapi? Sasa wewe unakuja kuzungumza tena, utukumbushe Tume ya Njonjo, Njonjo tulimchaguwa sisi?

**Com. Prof. Salim:** Endelea,

**Mr. Athumani Philip Ondasi:** Hatukumchaguwa sisi na hata hatutaki kusikia, tunataka kusikia nyinyi, wewe na wakubwa wenzake ambao sijui ndiyo Prof. Ghai, mumejanya u-professor wenu, mnaturudishia ardhi zilizoporwa. Ziziporudishwa mheshimiwa, natamuka hapa, huenda hata kesho nitakufa kwa sababu nimezeeka. Lakini zisiporudishwa, nina hakika hata yule anayetarajia kutawala, hata tawala sawa sawa. Kwa sababu hawa watu, haswa Likoni tuliyo nayo saa hii, wengi wao tunaitwa ma-squatter. Utasikia mzungu amenunua shamba kutoka Mariakani, we ondoka, wewe hiyo is ardhi yako. Ukirajibu kwenda kortini, korti inakuambia, mwenye cheti ndio mumilikaji, sawa au si sawa?

Haya ya mwisho mheshimiwa, je, umezungumza maneno mengi ya Katiba, sawa, tumeisikia, je, mahakama zetu zimetawaliwa na mtu anaitwa polisi au kikosi kinaitwa cha polisi? Nikizungumza hivyo mheshimiwa, mimi nimekwisha fungwa, robbery under violence/two, miezi sita, rumande, nafikiri unanielewa? Je, Katiba, hii ninazungumza sasa hii, au mnayoiongoza saa hii hii,

inazungumza nini kutusaidia masahibu hayo tuliyonayo kuhusiana na korti zetu? Asanteni.

*(Clapping)*

**Com. Prof. Salim:** Numbari ya tano. Majina kamili

**Mr. Juma Shabani Mohammed:** Jina langu naitwa Juma Shabani, Juma Shabani Mohammed, nimezakiliwa Likoni. Wazee *Asalaam Aleykum*. Mimi nafikiri sitazungumza yale wenzangu wamezungumza. Nina maneno kidogo katika hii Constitution, zilizo .....(Inaudible) tulizosoma au mimi nilipata kwa gazeti, kwamba .....(Inaudible) kidogo ambacho sijui kama kiliwezekana au la. Kesi yenyewe ni sarafu. Unajuwa katika nchi, kama vile tulizungumzia hii Katiba, kwamba kuna mambo mengine kidogo yamehusishwa, na zile ni common wealth countries za kisarafu. Sarafu ya Kenya nafikiri bado, ni ile ile. Nikija kesho, kesho kutwa Rais atachukuwa, mwingine naye, nafikiri sarafu, kwenye hiyo Katiba haingekuweko, tukaifanya sarafu ikiwa inaleta foundation peke yake, kwa sababu tukisema hivyo hii sarafu, huenda maRais kumi watakuwa .....(Inaudible) Kenya, pengine nasikia hivyo.

Naomba pia, kwa maoni yangu Tume itakapo kaa tena kujadili, hili swala la sarafu lifikiriwe sana, kwa sababu pia ni swala nyeti kiasi kwamba litatufanya Wakenya tuwe na sarafu tu. Ninakumbuka kama vile Amerika mpaka leo ni moja, kama vile ya Kiingereza leo ni moja tu. Naiombo hiyo, ndiyo yangu, ilikuwa sina mengi sana.

*(Clapping)*

**Com. Prof. Salim:** Nambari ya sita,

**Mr. Amin Kamala:** *Salam Aleykum..*

**Audience:** *Aleykum Salaam.*

**Mr. Amin Kamala:** Kwa jina naitwa Amin Kamala. Mheshimiwa kwenye Tume kwanza nina swala moja nataka niulize, nimesema kwanza kwamba ino Katiba inayopendekezwa hapa, kitu ambacho kinatokana wananchi wenyewe, lakini kulingana na vile ninavyo fahamu, naona kama sisi watu wa Likoni, tulipitishwa neno majimbo. Lakini naona ya kwamba umesema, Katiba ino mmependelea kwamba iwe na system administration. Je, kama sisi watu wa Likoni, tutapendelea system ya majimbo, itakuwa vipi? Je, ni maoni ya watu ama mlikuwa mmesha tengeneza Katiba lakini kufananisha maoni ya watu vile wanavyotaka, ama ilikuwa kuna Katiba ilivyo tayari?

Halafu la pili, ilikuwa ni kuhusiana na vile mmesema kulingana na wanawake katika ile Serikali itakayo kuja. Mmesema mnachanga katika watu mia moja, saa zile watakuwa wanatoa katika kila district, je, iwapo .....(Inaudible) tungekuwa

tumechaguwa kila district mwana mke mmoja, halafu ikitokezea kwamba wale sabini watijejee wanawake. Je, wale thelathini watakuwa vipi? Kwa hayo machache, .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Nambari ya saba.

**Mr. Ayub Masika Khaemba:** Majina yangu kamili naitwa Ayub Masika Khaemba, mkaaji wa Mtongwe. Mimi nina swala ambalo ningependa kuuliza. Mimi nina swali ambalo ningependa kuuliza Tume ya Katiba maanake, mmezungumzia mambo mengi mazuri, tumeyasikia lakini mimi kililio changu kilikuwa kwa upande wa, kwa hao watu ambao hawajiwezi. Haswa watu kama hawa waendawazimu, walemavu, visiwi na wengine. Kwa mfano mimi juzi, nilikuwa mahali, nikakuta kwamba kuna waenda zimu mahali, wanafukuzwa na police. Amani usiamini, walikuwa wanafukuzwa kutoka mahali ambapo walikuwa wamekaa kama maskini yao, wapelekwe sehemu zingine. Sijui walikuwa wanapelekwa wapi? Lakini, kwa upande kama Serikali yetu, watu kama hawa ambao hawajiwezi, hawajitambui, Katiba yetu inazingatia maisha yao kiviipi?

Kitu cha pili, nazungumzia kuhusu mazingira. Sisi tunavyo juwa kulingana na maisha ya mwanadamu, kitu mazingira ni kitu muhimu sana. Lakini tukiangalia Katika mazingira yetu, hiyo tunako kwenda, hasas mjini, utakuta kwamba kuna uchafu mwingi sana kimazingira. Unakuta mataka taka yamerundika mahali, yanaoza, ili kuonyesha kwamba, hewa na afya ya watu, pale itakuwa si nzuri. Hasa kwa upande wa Katiba, wanachukulia vipi kuweka mazingira yetu kuwa masafi kwa upande wa kule kama mijini?

Na kwa upande wa, pengine kama, misitu, unakuta miti inakatwa holela holela bila kuzingatia. Kuna ma-officers, kama ma-chief and DO, lakini utakuta kuwa kwamba, kuna area fulani unakuta miti imekatwa ovyo ovyo kama miembe, hata saa hii, unakatu kama minazi pia yakatwa ovyo ovyo. Ikiwa kama utakuja kusema, hii ndio itakuwa kutegemea sisi jamii yetu na ina katwa ovyo ovyo, Katiba inachukuwa hatua gani kuangalia vitu kama hivyo? Asanteni.

*(Clapping)*

**Com. Prof. Salim:** Nambari ya nane. Number eight.

**Mr. Juma Rashidi Mwaonja:** *Asalaam Aleykum.,*

**Audience:** *Aleykum Salaam.*

**Mr. Juma Rashidi Mwaunja:** Kwa jina naitwa Juma Rashidi Mwaunja kutoka Likoni.



**Com. Prof. Salim:** .....(Inaudible).

**Mr. Juma Rashidi Mwaunja:** Kwa jina naitwa Juma Rashidi Mwaunja kutoka Likoni. Nashukuru Katiba hii kwa kusema ukweli, ni ya mwelekeo kwa sababu imeanza na utangulizi. Utangulizi, lakini ubaya wake wamekosa kutaja wapagianaji uhuru kama vile wenzetu wa Afrika kusini. Kwa sababu kwa upande wa Africa kusini wamewaangalia zaidi wapiganiaji uhuru. Na ambapo hapo katika Katiba hii, sioni kama imetaja wapiganiaji uhuru.

Na pia, kwa upande wa watoto, nimesema hivi watoto wasitumiwe vibaya, lakini kwa upande mwingine ningesema kuwa kwani adhabu ni lazima ipatikane kwa watoto kwa sababu gani? Bila kumuadhibu mtoto, mtoto hawezi kunyooka, na kwa upande huu nimeona kuwa haikutajwa jambo la ajabu kwa mtoto kuwa ni lazima, isipokuwa adhabu lazima iwe ni ya kiwango fulani.

Na kwa upande mwingine, haikutaja, kuna mambo mengine kidogo, kwa upande wa walemavu, naona, halikutajwa hilo. Ambalo, pendekezo hilo ni kuwa,

**Speaker:** .....(Inaudible)

**Mr. Juma Rashidi Mwaunja:** Walemavu, kwa upande mwingine, hawakuzungumza pendekezo fulani ambazo ni muhimu ni pendekezo lakini kwa upande huo sikuiona kama limetajwa. Na pendekezo lenyewe ni kuwa, walemavu, tuliomba wasimamiwe jamii zao ki elimu na hata kimakao. Lakini kwa upande huo naona hapa hamkutaja.

Na pia kwa upande mwingine ni lawama mbona nalirukia moja kwa moji hii Tume. Tume kwa upande huu sema kuwa Tume haiko wazi, haiko wazi kwa sababu gani? Ni mimi nikiwa mmoja kwa wale ma 3Cs ambao walishughulika kueleemisha uraia, elimu ya uraia. Na mpaka muda huu, hatujaangaliwa chochote, ijapo shukurani wakatuambia chukueni hiki ni kitu fulani kwa ajili ya kuwashughulikia shuguli zenu, licha imekosekana, sisi tumetumika miezi minne bila kupata chochote. Kwa hivyo hili lawama nimelipokea ni hii hapa, nikiwa hapa nasimamia kwa naiba ya wenzangu kama kumi na tano. Kwa hivyo, tunalalamika kuwa Tume hii, ilifanya kazi nzuri sana, lakini ubaya wao ni kuwa ni haikuwa wazi ni kwa sababu ingetuangalia na chochote na ambapo wao wamejipangia marupu rupu yao na kisha tukipata chochote katika miezi minne hiyo, na mpaka dakika hii, na sisi kuna .....(Inaudible) wanaweza kushitakiwa wakati wowote kwa sababu katika miezi yote minne, hafuati na madeni. Je, madeni yao yatalipwa na nini?

*(Clapping)*

Hawana njia ya kulipa hizi pesa. Na madeni yao tungeyapata ili kwa ajili tu-afford tuwatumikie wao, na hatukupata chochote. Kwa hivyo naomba Bwana haina mtu, tuangalie sisi masikini, hatukupata chochote ila ni nauli tuliyokuwa tukiitumia. Asante.

**Com. Prof. Salim:** Number nine, number eight is written.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Majina.

**Mr. Abudi Mubarak:** *Salaaam Aleykum Waraha Matuhilahi Wbarakat.* Kwa jina naitwa Abudi Mubarak. Mimi bwana, malalamiko yangu ni kuhusu birth certificate. Na ninayo ushahidi wa kutosha sana kwa sababu mamangu mzazi, anayo birth certificate, na ameitoa hapa hapa Mombasa, nafikiri 1962. Mwanzo kutoka hii birth certificate, na hali kadhalika mimi mwenyewe ni nayo. Lakini naona ajabu mtoto wangu wa sita amepata lakini kuna kifungu fulani au note fulani hapa ameandikiwa kuwa mwenye kubeba karatasi hizi, hii ni mwananchi halasi, na ushahidi ni huu. Sina mengine zaidi isipokuwa ni hayo tu.

*(Clapping)*

**Com. Prof. Salim:** Asanteni sana kwa maswala yenu na maoni yenu, tumefurahi kweli tumalize hayo, kisha tukuje tena, DC hukuwa round ya pili. Bwana Mohammed Abdi alikuwa ametoa maoni tu bila kutaka kuuliza jambo lolote kwa hivyo tumemalizana naye, Bwana Mustafa ameuliza habari ya wale waakilishi watakao kwenda kuhudhuria mkutano huo mkubwa wa nchi hii, National Constitutional Conference, auliza ikiwa hawo wanaweza kutegemewa walala, na ikiwa walichaguliwa kwa njia iliyofaa.

Kwa hakika tulipopanga kazi hii ya kupata waakilishi, ilitibi kufikiria njia ya kuwachaguwa, tukaona kwamba local councils, makao yao au ofisi zao zitakuwa ni pande bora kufanya uchaguzi wa hao wawakilishi. Tutapanga kuwachaguwa hapo na tukasema kwamba katika kila district kuwe, kutoke watu watutu, mmoja awe ni mwanamke, mmoja awe ni ikiwezakena kuwe ni councilor, lakini si lazima, na watatu awe ni raia yeyote katika eneo hilo au district hiyo. Kwa hivyo tulifanya uchaguzi, tulitangaza katika magazeti kwamba uchaguzi huo utafanywa baada ya fulani tukaonyesha, tukasema, kwa mfano hapa Mombasa district, uchaguzi utafanywa baada fulani, tarehe fulani. Sasa ilikuwa si wajibu wetu tena baada ya hapo, kufanya lolote lile. Yamtegemea yule mwanamke ambaye ataka kusimama aje mbele aseme mimi nataka niwe mwakilishi, yamtegemea yule councilor hata mimi nitakuwa ndio councilor, na ya mtegemea raia yeyote wakati huu utamani kazi hii nataka ifanya, kwa hivyo nataka kuchaguliwa. Kutaka kuchaguliwa maanake upate watu, wafuasi wakuchaguwe. Councilor hakuwachaguwa hawa, natumia maneno hayo mawili kuchaguwa kuchaguwa lakini moja ni election. How they were elected, walipata wafuasi wale waliwachaguwa. Kwa hivyo tuliwachaguwa watu kwa kufuatia njia hiyo, na hao wafanyi kazi wetu, district coordinators wetu wa Mombasa ndio waliyosimamia, walikuwa ni returning officers. Na mpaka leo hatukupata mashataka yeyote kwa mfano Mombasa uchaguzi haukufanywa sawa sawa, au Malindi haukufanywa sawa sawa. Tulisema kwamba ikiwa mtu

hakufurahia, au aliona kwamba kuna hitilafu fulani ilifanywa katika uchaguzi wa waakilishi wa Mombasa au Malindi, au Kilifi na kadhalika, atuletea habari na sisi tutafanya unchunguzi kule Nairobi kuhusiana na agents wetu, au waakilishi wetu hawa, district coordinators. Na kwa hivyo kwa upande wa Mombasa hatukusikia lolote lasemwa, Kwale pia na kuingine hapa Pwani.

Kulikuwa na malalamiko kutoka maenoe mengine machache tu, na zingefanywa. Kwa hivyo sisi ni lazima tukubali wale ambao wamechaguliwa, kuwa wamechaguliwa wazi katika hadhara, hao twawapa umbele wafanye kazi yetu hawa.

Kisha aniuliza Bwana Sirahi, citizenship registration should be locally .....(Inaudible). Alisema kwamba, mimi nilisema kwamba registration itafanywa na Serikali ya kati. Nilisema kwamba citizenship, mambo ya kuhusu citizenship, yatafanywa na Serikali ya kati, na mambo ya immigration na Serikali ya kati. Lakini hii maanake sikuwa kwamba hakutakuwa na ma-ofisi hapa, tulisema kwamba ma-ofisi za serikali lazima zipatikane katika maeneo yote, kama hivi leo. Kwa hivyo immigration office ya hapa Mombasa itaendelea kutoa passport na kadhalika, kama nilivyosema. Muhimu ni kwamba mtu awe ni citizen.

Utapata mtu ni citizen na tumesema katika Katiba hii mtu atazingatiwa kuwa ni citizen au ni raia ikiwa au babake au mamake ni mzaliwa wa Kenya. Automatically yeye ni, ni raia na akiwa ni raia ana haki ya kupata passport, ni haki yake, kwa hivyo ikiwa Katiba hii itakubaliwa ikawa ndiyo sheria kubwa ya Kenya, mtu akiwa amezaliwa hapa Kenya, anayo certificate kusema kwamba amezaliwa hapa Kenya, pia ana certificate ya kusema kwamba mamake au babake amezaliwa hapa Kenya, ana haki ya uraia kwa hivyo ana haki pia ya passport. Pia ana ya ID, yote huenda pamoja. Katiba hii mpya itakwenda pamoja na haki tulizozitaja.

Na hapa afadhali nimjubi kabisa Bwana Yahaya hapa, kwa upande wake birth certificate na problem yake. Ikiwa Katiba hii, tuliopendekeza, itakubaliwa na national conference na Bunge, basi bila shaka certificate kama hiyo, birth certificate utaipata na itaonyesha kwamba huyu ni raia. Maanake birth certificate ndiyo nimeeleza kwamba ni mzaliwa wa hapa, na akiwa mzaliwa hapa na pia ana certificate ya mamake au babake kusema ni sawa pia ni wazaliwa hapa, basi huyu ana haki. Na akiwa hakupata haki hiyo, anaweza kushitaki mahakamani. Sheria yoyote iliyoko katika hii Katiba ikivunjwa na mtu yeyote ikiwa ni migration officer, or principal migration officer na kadhalika, mtu anaweza kushitaki kwalalamika kortini, atapata haki yake, sawa.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Nafikiri pia hatutaki kwamba hiyo certificate yasema kwamba huyu ingawa ana certificate lakini sina yote. Lakini ikiwa juu ya ile certificate, kuna certificate ya mama au baba, na ni mambo kama haya na malalamiko kama haya ambayo sisi imetufanya kubadilisha Katiba ilivyo hivi sasa. Na kusema kwamba mtu awe ni mzaliwa, mamake au babake awe ni mzaliwa akiwa na haki. Na akiwa ni raia hapo hapo, automatically, ana haki ya passport pia, na ID, pia ana haki. Na taabu ni kwamba wengi kati yetu hatujui haki zetu. Na hiyo ndiyo sababu ya sisi kuwa civic education providers na nishala hatutaendelea kuelembisha watu juu ya haki zao. Tumependekeza kwamba education Act isemwe kwamba, katika ile curriculum ya skuli, elimu

ya Constitution itiwepia ili watu wajuwe haki zao. Bora ni kwamba mtu ajuwe haki yake na aweze kupata msaada wakili kudai haki zake. Baada kuzijuwa haki zake, ikiwa wako sawa, adai haki, lazima tudai haki, tusilalamika peke yake, tuzidai zile haki.

Bwana Mwinyi Hamisi, wa democracy group, kwa hakika nimefahamu na wewe Bwana Mwinyi Hamisi kwamba democrasia huendelea kwa wajibu sana na kwamba hata nchi zilizo sifiwa kuwa zinaendelea sana, development, zimestawi kabisa pia wana taabu zao.

Na pia nakubaliana na wewe kwamba ardhi ni jambo muhimu sana. Lakini ni makosa kuwa kusema kwamba hatukusema lolote juu ya ardhi. Nimetaja habari ya Njonjo commission kama kuwakumbusha kwamba jambo hili ni kubwa hata ikawa Tume nzima imepelekwa kufanywa uchunguzi katika tatizo hili la ardhi na mashamba hapa nchini. Na atukisema kuwa sisi, hatukusema lolote juu ya ardhi, nimeeleza tuliyopendekeza hapa, tumesema kwamba matatizo yaliyoko, malalamiko ya wananchi lazima katika muda wa miaka miwili, Serikali ifanye uchunguzi. Katika malalamiko hayo, na pia kuyastawisha.

Pia nimesema kwamba squarters lazima wapewe makao. Kwa hiyo nafikiri sikufahamika uzuri hapo. Niikimtaja Njonjo, si maanake kwamba mimi au sisi Tume yetu haikufikiria au kzungumzia jambo hili. Tulizungumzia sana tena sana. Tumejuwa kwamba kuna taabu, tunajuwa kuna taabu, tunajuwa kuna malalamiko. Tunajuwa kwamba kuna ardhi zinazochukuliwa labda kwa njia ambayo si haki. Tutasema pia, kufanywe chunguzi katika ardhi ambazo wananchi wanasema kwamba zilichukuliwa kwa njia isiyo sawa. Na tukasema kwamba basi uchunguzi huu ikisikitika kwamba kweli hapa, kulitokea makosa, au hitilafu, au ardhi ya watu yalichukuliwa kwa njia isiyo halali, ardhi hizo, mashamba hayo yapokonywe wale watu ambao hawastahili kuwa nayo. Na tukasema kuwa wale squarters na landless wapawe makao, maanake ni kwamaba ardhi kama hizo zikichukuliwa na Serikali kutoka mikono ya wale ambao wamezipora, zitafaa hawa ambao hawana ardhi. Kwa hivyo tatizo hilo la landless wale squarters Tume ilizungumza, na tukasema katika muda wa miaka miwili, jambo hili litatuliwe. Na natumai kwamba, Bwana mwingi Hamisi na ndungu yetu Bwana Athumani, umefahamu kwa uzuri zaidi vile wamesema. Habari ya majimbo ilikuwa ile tumesikia kwamba watu watakao majimbo lakini tulifikiria sana jambo kama hili tukafikiria na gharama zake na kadhalika, tukaona

Na nitarudia kwa ajili ya kunasa maneno, ni kuwa kila neno linalosemwa hapa, lisisahauliwe na likumbukwe na li-record-iwe. Bwana Athumani ulisema kwamba mambo ya majimbo haikutajwa hapa, mlikuwa hapa mkachakuwa maoni yetu, tukasema kwamba tunataka majimbo. Lakini tufikirie kidogo, tulitaka majimbo kwa ajili gani, tulitaka majimbo ili tujihukumu nafasi zetu. Tujitawale kwa njia ambayo tutaona kwamba ina maslahi zaidi kwetu. Tutataka Serikali yetu iwe karibu zaidi. Ni watu ambao tatawafikia haraka. Kuwastakia na kupata mashataka yetu kisikizwa matatizo yetu kutotatuliwa. Kwa hivyo, tumefanya kazi hii kwa njia nyingine ya district councils. Utaona kwamba districts zikiwa na Serikali zake, zitakuwa ni karibu sana na wananchi, na mtawajuwa zaidi wajumbe wale mtakaopeleka kwenye baraza kwenye district council hawatasimamisha kamwe. Wale pia watakuwa ni wajumbe wenu. Na kwa hivyo nitaweza kuwafikia haraka.

Na tumesema kwamba district councils pia zina mamlaka, nikasoma mamlaka. Nikasoma mamlaka ya kila district council itapea watu kodi, pesa zile za kodi zitatumiwa katika shule, katika clinic, katika hospitali na huduma nyingine ambazo wananchi, maji watahakikisha kwamba maji wananchi wanapata. Ni mambo kama haya, basic needs, mahitaji ya kimsingi ya mwananchi ambayo sasa yakowa katika mikono ya district.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Ehe, nimeeleza hivyo kwa ukamilifu sana. Labda ulikuja ukapotelewa Bwana Athumani, lakini, yote hayo tumeyataja na kwa ajili ya upungufu wakati tu ndio wakaeleza kwa urefu zaidi. Fikira yangu ni kuwa kupitia idadi kubwa zaidi ya sura ili mfahamu kwa wingi zaidi yaliyomo katika, lakini yote hayo tumeyasema.

Pia kwa upande wa ardhi Bwana Athumani ulisema kwamba, hapa ardhi za wazungu, utuambie hii ni ardhi ya mzungu fulani, tokeni nyinyi. Tumesema kwamba yeyote ambaye si mwananchi, ardhi isipewe asiyekuwa mwananchi. Ardhi itakuwa ni ya wananchi na ni wananchi peke yao ambao watamiliki ardhi. Hivi mliponunua ardhi, mtu wa ajanab na mtu wa nje, aweza ku-lease, atapata lease.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Katiba inasema kwamba, ardhi ni ya wananchi. Lakini tumegawanya, ardhi ni ya aina tatu. Kuna state land, siyo? Hiyo ni ya area ile. Kuna na public land ambayo ni ya serikali ya juu, ambayo baada ya ukoloni kuondoka, ili hand over kama serikali ya kati ya Nairobi. Basi pia kuna individual land, mamlaka yake mtu, ni yake na ya mababu zake na kadhalika, hiyo ni private land. Maanake hapo private pia hata watu wa Likoni hawawezi kuingilia sehemu yeyote, ikiwa ni ardhi yako Bwana

Athumani, ndugu yako mwingine, hapa hapa hawezi kuingilia. Bwana Mubarak pale hawezi kuingilia. Kuna private, kuna na public land. Kisha kuna na Trustland. Trustland ya jamii katika eneo hili. Kwa hivyo, na tukasema kwamba ardhi ni milk ya Wakenya peke yake. Na ikiwa ni public land, Serikali ya juu pia iweke au ihifadhi public land kwa masalahi ya wananchi, na isitolewe ovyo. Na kwa ajili ya kuwa kwa wakati kuwa hatuna, tumesema kuwa kwamba kuwe na land commission. Ile ya Nairobi, infact ile, siyo ya Nairobi ile. Kuwe na commission ambayo itahakikisha kwamba ardhi ya wananchi isitolewe bila ya kujulikana imetolewa kwa nani, na kwa ajili ya kitu gani.

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Land commission ni Tume, idadi kadha ya watu. Watakuweko kwenye Tume hii. Si land commissioner, or commissioner of land la, hii ni land commission kwa nchi nzima kuhakikisha kwamba ardhi ya wananchi iko salama. Na haitolew kwa .....(Inaudible) na hakuna mtu mmoja ambaye atatoa ardhi kwa mtu yeyote mwenyewe. No one person,

hakuna mtu mmoja binafsi, ambaye atakuwa na haki ya kutoa ardhi kwa kumpa mtu mwingine. Jinsi haya yako, tumeyafikiria.

Pia Bwana ulisema habari ya police, pia tulizungumza hayo. Nafikiri kwamba tatasema kwamba, binadamu, mwananchi wa raia ana ya kuondoka, kuingia huku na pale, kuenda bara barani, bila kusimamishwa na anakuambia fanya hivi, fanya hivi, fanya vile. Na kwa hivyo, hana haki ya kukusimamisha. Ikiwa, lakini tunafikiria ya kwamba ikiwa Katiba hii itakubaliwa, au mswada huu wa Katiba utakubaliwa, kuwa ni sheria, haki ya binadamu, haki ya mwananchi, pia asiingiliwe nyumbani kwake. Akafanyiwa inspection ya nyumba yake, masanduku yake na nguo zake, zikatupwa hapa na pale. Kwa hivyo mambo haya ya polisi. Mungu akipenda, yataondolewa chini ya Katiba. Na mtu ana haki kumshitaki mtu atakaye fanya hivyo.

Pia tulisema kuwa mtu akishitakiwa, akishikwa, anapelekwa, anapigwa na kila kitu, jela, mambo haya pia tunaondoa. Tumezungumza kwa urefu kidogo ujuwe jinsi ambavyo mtu hushitakiwa lazima haki zake zihifadhiwa, bill of rights, asipigwe ovyo, asiingilizwe katika cell akapigwa na mtu. Afanye chakula, akisha hifadhiwa na wakili apawe wakili kwa gharama ya Serikali ikiwa hana pesa za kutosha. Aingizwe katika hali aweze kuoga, apewe chakula na kila kitu, saa ile yuko remande. Saa hizo ile treatment, ya mshitakuwa tumelezwa kwa urefu haya na ningependa wenzetu wote, Bwana Stanley wenzako wote, wapate nafasi kupitia mswada huu wa Katiba katika ofisi yetu kila mtu apate copy na ikiwa kila mtu ameshapata copy zaidi, na muweze kupata copies hizo mkifika kule district documentation center yetu. Kikao cha taarifa zetu ziko pale national library Mombasa. Mungu akipenda mtapata copies hizi za taarifa hii.

Pia tulichapisha you know, mswada huu wa Katiba katika Naation, katika Standard, katika People, ili kwamba mtu akinunua siku ile atakayo nunuwa Nation, atapata mswada mzima, neno la kwanza mpaka neno la mwisho katika gazeti bila kulipa zaidi. Ndio ilikuwa njia ya rahisi, lakini sisi tumewapa pesa nyingi sana hawa wenye magazeti. Kwenye kuchapisha kwa advert moja, ilani moja fupi, gharama ya shilingi siyo elfu ishirini thelathini arobanne. Kwa hivyo, hii nzima taarifa hii ni draft nzima kuitia kwenye gazeti kwenye gharama kubwa. Lakini lengo ni kwamba mwananchi akinunua Nation, akinunua Standard, akinunua People newspaper, atakuwa wakati huo samahani, wakati huo ameshapata pia na copy ya mswada wake. Kwa hivyo tulifanya kazi kadiri tuwezavyo, kuwapatisha wananchi, lakini hata hivyo, documentation center yetu itakuwa na colour za kutosha mwananchi ikiwa kwa term, na term kwenda kusoma pale atakaposoma.

Na pia tuomba kwamba mtupe maoni yenu baada ya kusoma, tupata kubadilisha. Kama nimesema hapo awali, sisi ni binadamu, si malaika. Tunaupungufu wetu pia kama binadamu. Ikiwa tumefanya upungufu hapa na pale, mtupe maoni yenu. Waakilishi wenu mmoja wao wa Mombasa district yuko hapa leo, na Bi Amina, hebu simama Bi Amina? Yeye ni kati ya wale waochaguliwa, mmuendee mmpe maoni yenu juu ya jambo lolote, mkimpa, mtaweza kumpata.

Alikuweko Councilor pia, kwa hivyo, ni wajibu wenu na pia ni haki yenu kutupa maoni yenu juu ya mswada huu, si wa mwisho. Na kama nimesema hata ikiwa nyinyi mlukubali, au kutokubali, Katiba hii tuliandika, national conference pia lazima ikubali kabla

ya kuwa sheria. Kwa hivyo lazima muwashawishi, kwa hivyo lazima muwashawishi wale wajumbe wenu na waakilishi wenu, waikubali, ikiwa nyinyi, au waambie, mkienda kule, jaribuni kubadilisha jambo hili kwa sababu hii na hii na hii. Ili kwamba mwishowe, tupate Katiba ambayo itapendekeza kila mtu. Inapendwa na kila mtu. Hiyo ndiyo nia yetu tangu mwanzo, kwamba hii Katiba itakuwa, Katiba ambayo itahudumia wananchi wote kwa jumla, kwa njia itakayofaa na kuwapa haki zao na mahitaji ya ki msingi, halafu hala kalu. Ikiwa ni chini chini kabisa mtu apate haki zake za kutoa haja zake za kidini. Elimu ya kutosha, amani ya mbuyu wake na jamii yake, na nyumba yake, chakula cha kutosha, matibabu ya kutosha, mazingara mazuri.

Kuna jamaa mmoja aliuliza habari ya mazingara, pia yako, kuna sura nzima juu ya mazingira hapa, na jinsi ya kulinda mazingara, na jinsi ya kulinda mazingira. Na wajibu wa kila raia kulinda, pia adhabu kwa wale ambao watachafuwa mazingara, yote haya tumeyasema katika mswada. Ni chapter, sura ya kumi na mbili, iko hapa.

Bwana Juma Shabani ulitoa maoni yako na maoni hayo tuliyasikia hapo awali yasarafu na jinsi ambavyo itakuwa ni gharama kubwa ku kufikiria jambo hili. Nataka mkumbuke kuwa mbali na hii Katiba, tuna taarifa, report, report ya kazi zetu, na wanachi waliyotuongia juu ya kila jambo.

Na habari ya sarafu pia wananchi wengi wamesema kwamba, ni gharama kubwa kwa nchi yetu kwa kubadilisha sura za kila Rais. Kwa hivyo hili liko katika report yetu, mtaiona, pia, hii ni summary, ni report au ni taarifa ya kifupi kabisa.

Kutakuwa na taarif kurasa sijui elfu ngapi, majalada nane, nane, .....(Inaudible) ni twenty five, inataarifa kubwa kabisa, maelezo marefu zaidi. Kwa hivyo, ikiwa hawa jamaa waakilishi wenu na wajumbe watakao hudhuria, national conference wataitisha ile pia huenda ikatiwa kwenye hii Katiba. Ni kweli .....(Inaudible) habari ni kwamba iwe ni moja, everything is there. So, ikiwa jamaa wengine wanahisi kwamba ni jambo mhimu, watu washawishi waakilishi wabadilishie na waseme kwamba lazima kwa mfano, kwa mfano tu, rais iwe ameshakufa kwa zaidi ya miaka kadha kabla ya sura kutumiwa katika sarafu. Amerika, ni zaidi ya rais mmoja picha yake iko katika sarafu, si mmoja tu. Kuna Lincon pale, kuna Washington, na watatu wale wengine, na walingojea mpaka mtu akisha kufa inakumbukwa na kila kitu, na kukumbuka utumishi wake kwa uma, ndio .....(Inaudible).

Amin Kamala, majimbo is not there, kweli, tushaeleza sababu yake, na wameuliza yeye. Hii Katiba ni kama watu walivyopendelea, mimi naweza kusema kwamba mapendekezo yetu kwa hakika ni mapendekezo yale ambayo inatokana na watu. Si mapendekezo yeyote, ingekuwa tutafwata mapendekezo ya kila mmoja wetu aliyotupa, mapendekezo mengine hugongana siyo? Pendekezo langu mimi litakuwa labda tofauti na pendekezo lake. Sasa tulikuwa na nani? Lazima liweko pendekezo moja tu katika kila kitu.

Kisha aliuliza, mlisema kwamba katika national council, ile nyumba moja ya,

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Yaah, na pia tumenasa maoni ya wananchi katika kila constituency, tumeandika taarifa yale tuliyasikia na maoni tuliyoyapata, kutoka kila constituency. Kuna report moja kwa kila constituency. Sijui kama tunayo sample ya hapa, kuwaonyesha kwamba tunayo Changamwe, tunayo Kisauni, .....(Inaudible).

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Kwa mfano hii ni taarifa au report ya maoni tuliosikia constituency gani hapa?

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Hii ya Changamwe na kadhalika, kila constituency ina report yake Copies za report hizi mkitaka muweze kusoma report ya Likoni katika ofisi yetu, documentation center hapa katika library niliyowaambia hapa mjini Mombasa.

Na ameuliza Bwana Amin Kamal kuhusu wananawake, asema watukuwemo, mlisema kwamba mtawapa viti thelathini, je, katika vile viti vingine, ikiwa wamepata viti pia, mtafanya vipi? Tukasema jawabu ni kwamba watu wengi, hakuna ubaya, ikiwa ni zaidi ya thelathini. Tunataka kila mwananchi, kila raia awe na uwezo, wa kuhudumu nchi ni Ikiwa ni mwanamke au mwana mme. Ikiwa ana uwezo na huyu amechaguliwa na huyu amechaguliwa katika uchaguzi kutakuwa na wale waliyomchaguwa wale waliyochaguwa wakijua ana uwezo, siyo? So, why not, kwa nini hatumruhusu kuwa katika national assembly na pia katika national council?

Ayub Masika Khaemba umesema kwamba wazee na jamaa na ambao akili zao zimewapotea na walemavu tuwafanye nini? Kwa hakika pia ukisoma mswada wa Katiba tumewafikiria wote hawo. Nafikiri labda ulichelewa kufika lakini wale wenzako waliyokuwako, nafikiri watakumbuka ndio waseme habari ya wazee. Nasi senior citizen ambao ni wajibu wa Serikali na wajibu wetu sisi, ikiwa ni jamii, kuwafikiria na kuhakisha kwamba, maisha yao ni ya sahali na si ya taabu sana. Mad persons pia, kila mwananchi tumesema kwamba ana haki ya kupata, kuwa na treatment inayostahili, na hili ni jambo ambalo linahusu matibabu, mtu ambaye akili yake imemruka, huyu anahitajia matibabu Tumesema kwamba basic needs, haja ya chini kabisa ya mwananchi ni kati ya haja zake ni matibabu. Kwa hivyo huyu pia ataweza kupata matibabu asaidiwe.

Ndizo hizo tumezungumza, kwa hakika nimezungumza kwa ufupi sana lakini kuna maelezo mengi zaidi kuhakikisha kwamba mlemavu ana haki ya kupatiwa kazi sawa sawa na asiyekuwa mlemavu tumesema kwamba accessibility, uwezo wake wa kufika ambapo ataka kwenda iwe ni rahisi zaidi. Katika majengo makubwa marefu, mambo yale, mambo ya matatu pia, ukifika kule uingereza buses zao, utaona kwamba kuna ngazi maalum kwa walemavu kupanda basi, na hawana basi maalum. Wanapanda basi kama zile zao. Huduma zote hizi nitasema kwamba lazima wapee walemavu ili maisha yao yawe rahisi zaidi. Na pia



washirikishwe katika utawala wa nchi, katika kila stage, katika councils, katika Bunge pia. Tumesema kwamba kila party jambo ambalo tulilitaja, kila chama cha kisiasa, katika list yake ya wale ambao tutawapeleka mbele kama candidates, lazima wawemo walemavu na youth katika list hiyo na akina mama. Wajaribu kuweka mbele katika list yao.

Na tuombe kwamba jambo hili litafanywa, hivi sasa tunaye Bi Asiyo ambaye bila shaka mnamjuwa ni MP, na tanaomba kwamba jambo kama hili litaendelea kukuwa zaidi. Mwajuwa jambo lingine ambalo mimi nalisema sana ni kwamba, kurekebisha Katiba ni kitu kimoja, kurekebisha akili za watu na nyoyo za watu ni kitu kingine pia. Na msione kwamba Katiba hii ikipitishwa kesho, mambo yote itabadilika yakawa mazuri, la, lazima yule policeman, askari abadilishwe akili yake, ibadilishwe ile training yake, isomeshwe juu ya haki ya mwananchi, hata kumuita, kwa njia ya kiiungwana mwananchi, Uingereza kule, askari hamuiti mtu ati, njoo hapa, hamuiti haswa, mama, hamuiti madam, ikiwa ni mwanamke. Mambo kama haya yachukuwa wadhifa kubadilika. Lakini lazima tufanye kama tuwezavyo, kubadilisha, kurekebisha Katiba. Tukirebisha sisi, kama raia na tuwa-train watoto wetu kwa njia ambayo wawo pia watajuwa haki zao. Na pia watajuwa haki za wenzao, ili kwamba new generation ndio policemen, new generations of children, new generations of leaders, watakuwa katika hali ya juu kabisa.

Nafikiri nimejibu kwa kukutosha hapo, Bwana Juma Rashidi, Preamble nimesema kwamba ina-mention kwa kuwa ile nafasi nitakubaliwa na wewe, na kubaliwana na wewe, kwa hakika tumebishana sana juu ya Preamble, tumepata mapendekezo mengi, mapendekezo mengine akisema kwamba freedom fighters should be mentioned. Tuseme kwamba the .....(Inaudible) they deserve to be mentioned. Lakini normally preamble kwa desturi huwa ni fupi sana, na hatuwezi kutia kila kitu hapo. Na huenda ikabadilika pia, huenda freedom fighters mwishowe ndio wakatajua katika hiyo Preamble ya mwisho, lakini it was a case of knowing kujuwa lini nilipi kutia kwenye Preamble, na ni lipi kuliwacha nje.

Children, nafikiri ukiisome uzuri kwamba vile tulisema kwamba watoto wako na uhuru wao sikuwa hatutaki wawe disciplined children. Lakini twafikiria, ile discipline pia isiwe ya very poor. Isipite mpaka. Na tukigharamisha sisi, adhabu ya kumpa mtoto, kumfanya mraia wa halali hii ya bona fide, lakini kuna haramisha mtoto kuadhibiwa na mzazi wake. Kuchukuwa gogo nyumbani, kuenda nayo huko akipigwa. Hiyo, discipline, si adhabu. Hiyo ni adhabu, na sisi tunaharamisha adhabu kumuadhibisha mtoto, kumlazimisha afanye kazi, saa nyingi sana katika garage au, tangu asabuhi mpaka usiku huyu yuko pale Likoni ferry auza njugu na kadhalika, hata hakupewa chakula siku hiyo. Hakupelekwa skuli. Fees iko lakini hakupelekwa, lakini kwa kuwa wazazi wataka pesa, pesa kuwa ni bora zaidi. Kwa hivyo haki ya mtoto, lazima tuifikirie adhabu utampa lakini pia utampa haki zake za mavazi elimu, matibabu, na kadhalika.

Disabled tumewataja kwa urefu sana, ningependa waanze kueleza zaidi, na tumesema kwamba nao jamii yao wasaidie.

.....(Inaudible) nimezungumza hapa na wenzangu hapa wamesema kwamba yale malipo ambayo .....(Inaudible) tumewapa, kweli hatuweza .....(Inaudible) watakavyo wao, kwa kuwa pesa, haziwezi kutosha, lakini, ni jambo ambalo

tunaweza kulichungulia zaidi, na ikiwa mtu akidhulumiwa kwa kupaa haki yake, tuatamuomba atalettee barua yake, atueleze, utafanya kazi gani, jamaa hawa wasifikishwe kwa ile kazi amefanya, lakini hakupewe hata ndururu, na tutajaribu kurekebisha mambo hapo. Bwana Yahya nafikiri nishamalizana nayo. Shukrani. Samahani, nimejibu kwa urefu hapo, lakini ilikuwa ni muhimu, tasameane sana. Tuko katika stage muhimu sana, na ni muhimu kupata maoni yenu na malalamiko yenu pia ili tusaaidiane.

Sasa nitachukuwa nafikiri kwa ajili ya wakati, na tuna mikutano mingine, watu watano tu, one, two, three, four, five. Na wengine tafadhalini ikiwa mtaweza kufika kesho kutwa tuko Chandaria Hall, Mombasa. Kwa ufupi Bwana.

**Mr. Maalim Jamal:** Majina kamili mimi Maalim Jamal, mzaliwa wa Mtongwe. Swali langu mimi ninalouliza ni swali moja tu, muhimu sana kwa ufupi. Kwamba kushapewa kitu, kwamba .....(Inaudible) hii shamba, .....(Inaudible) unayo, hiyo shamba ukisha pewa ni yako? Kisha uwezaje kusema hiyo hiyo kasha uambiwe na county council ya kwamba uilipie ndio uambiwe na county council ya kwamba uilipie, na kama hukulipa, itauzwa, na wewe utaruka patupu. Na ili hali uwe maskini, je, hapo serikali au tuseme hii tume, itapoangalia hapo maanake hatujasikia hili swali likigusiwa. Mnasema hakuwezi kuwa kwa njia zaidi, mengi zaidi,

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Mr. Maalim Jamal:** Wameshapewa shamba, kitu ulishaambiwa ni chako, lakini kile kitu ambacho ni chako, utaambiwa, lazima ukilipie, na kama hukilipii kitauzwa, leo uruke. Sasa kina maana gani? Ni chako hicho?

*(Clapping)*

**Com. Prof. Salim:** Wapili?

**Mr. Philip Muremo Jagelo:** Kwa jina naitwa Philip Muremo Jagelo, mkaazi wa Likoni. Swali langu hasa, linahusu chapter 4A, kuhusu mshahara, tuseme kabisa kuhusiana na mambo ya labour. Bwana Prof. mimi sijaridhika kabisa na nakala hii kwa sababu mumesema kwamba katika nakala hii, kutakuwa na commission, ama Tume ya kushugulikia haya mambo. Mimi naona hii kitu ni framework sawa sawa na hii, Katiba tuliyonayo ni ya zamani. Tukiangalia mambo ya labour Bwana Prof. tunao watu ambao wanahusika kushugulikia Wakenya walio, au wanaonyanyaswa kimshahara. Ofisi hii ina watu vile vile ni Wakenya ambao wanaolipwa na ushuru wa wananchi kushugulikia watu kunyanyaswa kwa mishahara. Bwana Prof. kuna rampant offences, ambazo zinakuwa classified kama .....(Inaudible) servants. Kwa sababu ya kutolipwa mshahara ya kisawa sawa. Kwa hivyo mngesema kwamba kutakuwa na Tume, sina imani hawa Tume watakuwa ni watu tofauti gani na wale ambao wako in place sasa, ambao wanazidi kunyanyasa Wakenya. Ukiwapelekea case pale kwa labour umenyanyaswa na tajari, yule tajari anaenda anazunguka, wanakula naye wewe umebaki wateseka. So, mumeweka tools gani in place kwa kuhakikisha

kwamba, mkenya yeyote aliyethulumiwa kimshahara atapata msaada wake namna maanake binadamu ni wale wale na ni sisi sisi?

La pili, Bwana Prof. tukiangalia mambo ya foreign investors, Kenya hapa sisi ni watu ambao ni wakaribishaji, tumekaribisha watu, wamefunguwa vibanda vyao hapa vya kazi, makampuni. Mimi nina enough evidence ya kampuni fulani ambayo imechukuliwa, imefunguliwa na mtu fulani na amatoa ndugu zake, jamaa zake huko nje, ndio wanafanya kazi, katika kampuni hiyo, na pia kuna waafrika wakenya wenzetu, mnaweza kufanya kazi, ngazi moja the same category, the same job group. Lakini yule mtu yuko kwa sababu anatoka huko nje, in a week's time amenunua gari, anakaa nyali, na wewe wakaa kuhu, huku, Likoni, hata biaskeli uwezi kuji nunulia. Kwa nini tusiwe, tusipewe mshahara sawa katika zile ngazi za kazi tunafanya pamoja na hawa watu. Ikiwa ni mhindu, ikiwa ni mzungu yeye ni manager, mimi ni manager, msahara iwe sawa, kama anaweza kujinunulia gari, na mimi niweze kujinunulia gari.

La tatu, Kenya hii Bwana prof. kuna mawakili, mara nyingi kunazo ma-cases zaidi ya ma elfu ya ma wakili kuthulumu wananchi. Mawakili wamethulumu wananchi, cases ambazo zinawakilishwa kortini zinafanywa, vyeti vinatolewa, zinalipwa, mtu atazungushwa miaka nenda rudi, miaka nenda rudi, miaka nenda rudi, hapati haki yake. Ile body ambayo imechaguliwa kushugulikia maswala haya, inaitwa the complaints commission, Monrovia street, Nairobi. Bwana Prof. hawa wa mama wakongwe watoke hapa Mombasa, wafuate mambo ya case ya Nairobi, na wale ni waakili wenziwo, polisi ashafungwa mkono, case na waakili usiingilie, nenda kwa complains commission. Nyinyi mnasema katika nakala, there would be a legal bond ambayo itakuwa imelipwa na Serikali ama nini kushugulikia wale ambao hawawezi kugharamia wakili. Ina utofauti gani na wale complains commission ambayo pia wakish chukuwa case, wafanya uchunguzi wawo wa miaka mitatu kisha wanakuambia, nenda uchukuwa wakili mwingine umstaki huyu wakili? Yaani, case, ya nyani upeleke kwa korti ya tumbili, siwezi kushinda hiyo.

**Com. Prof. Salim:** .....(Inaudible).

**Mr. Philip Oremo Jagelo:** Nimemaliza Bwana Professor.

**Mr. Bakari Salim Gandi:** Mimi kwa jina naitwa Bakari Salim Gandi. Kwa kusema ukweli hii Katiba ni nzuri sana, na tumefurahika sana, lakini swala langu ni kwamba, sisi Katiba tumeipenda, lakini kuna majihapa wengine Katiba hawaitaki. Je, sisi, tuliyoienda Kenya, kwa sababu hii Katiba ya Kenya siyo ya watu binafsi, tutafanya aje?

**Mr. Musa Mohammed Bakari:** Mabibi na Bwana *Salaam Aleykum*.

**Audience:** *Aleykum Msalaam*.

**Mr. Musa Mohammed Bakari:** Mimi maoni yangu ni kidogo. Jina langu ni Musa Mohammed Bakari, .....(Inaudible).

Nasikia haya maswala yangu niyonayo mimi ni kuhusu kazi, sisi kama watu wa coast hapa, ikiwa kutatokea kazi hapa, huwa kutachukuliwa watu wengine kama sima nini katika kuchukuwa nafasi hapa, alafu sisi watoto wetu watakwenda wapi? Kwa hivyo katika Katiba ingine, palipo na kazi watu wa pale wafanye kazi yao.

Jambo la pili, ardhi .....(Inaudible) kila siku tuungane katika majumba haya, katika majumba haya lakini kutoka utotoni, kutoka baba zetu mpaka sisi, ardhi hii ni ya nani?

Jambo la tatu, ni utalii unaofanya katika sehemu hizi, .....(Inaudible) zile zitolewa hapa hapa zifanywa makisudi na ma-hospitali, zitafuliwe tena pesa nyingi. Kwa hayo asante.

**Mr. Matano Ramadhani:** Kwa jina naitwa Matano Ramadhani. Swali langu ni ku, ningependa kujua ya kwamba mjumbe akisha chaguliwa baada ya miaka kumi, yaweza kurudi tena akachaguliwa kama waziri ama anaweza kuwa amemaliza mambo yake. Mbunge, amesimama vipindi vyake ni viwili, akishatoka kile kipindi cha tatu, inasemekana kuwa waziri atachaguliwa from nowhere, siyo Mbunge, yaah, sasa yule mbunge akimaliza miaka kumi, anaweza tena kurejeshwa kama waziri ama la?

**Ms. Aziza Abdala:** Kwa majina naitwa Aziza Abdala, mimi ni katika hicho kitabu cha Katiba mpya, au katika maoni tuliyotoa, kuna hii mambo ya Mazrui Land Trust of 1931, kusema kweli hii act kwa nini haiwezi kubadilishwa, maanake mimi naona watu wakisema matatizo ya land, lakini ingeondolewa hii kipeke cha Mazrui, kiwe hakiko maanake hayo Mazrui siyo kujadili hapa Kenya mpaka wawe watakuwa na kipenge katika Katiba baado tutawagai, kwamba na PC mwenye kiti wa hiyo format yao. Kwa hivyo, hiyo act twataka iondolewe maanake hawa Mazrui wana land kubwa sana, ambayo sisi wanaKenya, tuko ma-squartr, hatupati land, na .....(Inaudible) mapaka watu wawe ni wa Mazrui. Kwa hivyo, hiyo nilikuwa nataka iwe nitashugulikiwa. Kwa hayo asanteni.

**Ms. Mwana Kombo Juma:** Akina mama walia sana. Mimi kwa jina naitwa Mwana Kombo Juma Mwagomba, mimi nasema hivi, mbali vile wenzangu waliponituma sina mama, na watoto wangu, kwani mimi nina watoto wengi maanake hata huko bara pia kuna, hii Katiba kila mmoja yuaitaka, na imependeza sana, kwa sababu mumezata kwanza .....(Inaudible) kututumikia. Lakini hivi niliyokuja, kama mngokuja na Katiba ya majimbo, nina hakika nyinyi mngekaribishwa vizuri na mngengebwa na mngokuwa na furaha na kubwa sana. Kwa sababu nakuambia hii Pwani nzima, mpaka hawa wenzetu, wanaojukumu kuu, Kenya watapata majimbo, hakuna jambo lingine linalo takikana, majimbo tu. Hapa nchi hii hakutakuwa na .....(Inaudible) lakini kwa kusema ukweli sisi hapa sisi watu wa hapa kwetu, kwa kusema kweli, tukisema coast ni Malindi, Kwale, na pengine kwa, tuseme, lakini ni majimbo tu. Basi, halina kitu kingine twataka, na tulivyojitolea, tunaamini kwamba tutapata majimbo, sawa? .....(Inaudible). Asanteni.

**Com. Prof. Salim:** Shukrani kwa swala zenu na mapendekezo yenu, tumeandika, tumenasa kwenye tape, lakini .....(Inaudible) ya hapo ni kama ifuatavyo, nitajaribu kujibu kama niwezaavyo. Bwana Maalimu Jabal ulizungumza habari

ya mtu kuwa na shamba au ardhi, akapata na title deed. Kisha akaambiwa pia utalipwa malipo fulani. Kwa hakika iliyo kuwa kote ulimwenguni mtu akiwa ardhi hua analipa. Kitu fulani ili kwamba maanake kuna utumishi wa kiserikali, ambao unafika kwenye ardhi yako kama maji na kadhalika. Kwa hivyo hao jamaa wanasema kwamba, kuna haja ya malipo fulani ili huduma hiyo iendelee, uendelee kuipata. Sasa .....(Inaudible) wanasema kwamba title deed ni karatasi inachapishwa na inatayarishwa, hiyo inahuduma fulani na gharama fulani. Hiyo ndiyo sababu ya chief, ingawa ukisoma report yetu, tumezumzia lalamiko hili la wananchi. Tumesikia mahala pengi sana, nikisha pata title deed ardhi ni yangu, kwa nini niendelee kulipa fees na kadhalika. Tume litaja katika report yetu, na sasa inategemea katika hiyo conference, watakavyo kata shauri ikiwa wataondoa au watabakisha, fees ambazo, au rent ambayo tunaambiwa tulipe.

Bwana Philip Oremo umezungumza habari ya labour na jinsi malalamiko yalivyo, pia tunafahamu sana, tumesikia malalamiko hayo, tumesoma magazetini, Bwana Twoli akizugnumza juu ya wafanyi kazi na pia juu ya investors na haja ya kuwa shawishi waje kwa wingi zaidi tupate kazi nyingi zaidi na kwamba hatukutaja mambo hayo katika Katiba.

Tumetaja habari ya wafanyi kazi, na wafanyi kazi kuwa na haki ya kupata mshahara wa kutosha. I don't know whether you have come across them. Ulio nayo hapo kwa hakika ni taarifa, na tena hiyo ni taarifa fupi, lakini au report, hiyo ni summary report, lakini kuna na report kubwa zaidi. Na zaidi ya hivyo, constitution enyewe siyo hiyo, draft constitution ni hii. Nafikiri hujapata nakala, kwa hivyo nasikitika kwamba hatakuwa na nakala za kutosha, kumpa kila mmoja, lakini kutakuja na, kutakuwa na nakala nyingine zaidi kutoka Nairobi, zinawekupatikana baada ya siku chache katika documentation centre yetu hapo Mombasa.

Na katika mswasda wetu tumetaja kwamba every worker has the right to fair remuneration, fair means, fair. Unajuwa watu wengi hatuwezi sema hapa kila mfanyi kazi katika category apate shilingi elfu tatu, hii ni Katiba ambayo tutatumai kwamba itabaki na sisi, kwa muda mrefu sana. Eflu tatu kabla ya miaka ishirini ilikuwa ni pesa nyingi sana. Tukiandika elfu tatu baada ya miaka ishirini nyingine, elfu tatu ni kama shilingi mia tatu au shilling thelathini.

Lakini tunasema fair, ikiwa .....(Inaudible) na hiyo tumesema.....(Inaudible). Kwa hivyo na tukumbuke pia, hii ni sheria kubwa, ni kama sheria nzee. Kisha kuna mzee ana watoto, kuna sherehe nyingi ambazo zafanywa, labour act na mambo kama hayo, kwa hivyo katika hiyo labour act, twatumai ya kwamba Serikali itafikiria jambo kama hili, na malalamiko ya hawo uliowaleta, si ya leo au ya jina au ya juzi, ni ya siku nyingi sana. Na tunafahamu sana tukiwa na wananchi, kwamba wafanyi kazi wengi mshahara wao uko chini sana.

Kwa hivyo twataraji kwamba katika mabadiliko yatakayofanywa, katika kanuni nyinyine, ambao itafuatia kanuni hii kubwa ya au kanuni nzee, yatafikiria jambo kama hili. Nayo yataimplement jambo hili la fair remuneration for workers. Tunasema they should have fair remuneration, for the ideal working conditions. Tunajuwa wafanyi kazi wengine wanafanya kazi katika hali mbaya sana, hali ya hatari kwa afya yao na kadhalika. These are details, hayo ni mambo ya details lazima iweko katika sheria ndogo. This is the parent law, it should be retired law. Ambako mambo kama hayo itafanyika, must depend on the

Government. Ndio kutakuwa na labour, ministry of labour, ambao itabadilisha sheria zote zinazohusikana na wafanyi kazi na kadhalika.

Kwa hivyo, I can say, foreign investors, tumesema kwamba katika Katiba kwamba kuna haja ya kuwa na mahusiano mazuri, na nchi nyingine, we should be a good citizen of the world, na related to that we should be relations with other nation and that includes things that foreign investors. But again the details of how, au vipi tunaweza kuwashawishi waje hapa, is a matter of some other ministry or some other agency, to work on the details for that work.

Lawyers, mumeshitaki kwamba wengi wao kwa hakika ni watu ambao hawana pesa wale ambao wamekodisha kuwafanyiwa kazi, na ni jambo ambalo tumelifikiria. In fact it was a turn ingawa tumezungumzia habari ya mahakimu na kadhalika, tutakuwa wenzetu wengine ambao nimesema kwamba pia kuna haja ya uchunguzi wa lawyers. Lakini hata hivyo, tuna commission zingine tatu, ambazo zinahusika na kuhakikisha kwamba kila mtu ambaye anahudumu mwananchi, lazima ahudumu kwa njia iliyo sawa. Na ukiona hapa kwenye page, 14 ya draft Constitution, kuna commission inaitwa, commission on human rights and admission of justice. Mtu anaweza kushitaki kwenye commission hii lawyer yeyote. Mbali na hayo, kuna integrity, ethics and integrity commission, kama nilivyo eleza ndugu zetu hapo awali, hii ni commission ambayo itachunguzwa conduct, ya kila anayehudumia mwananchi, na ikiwa yeyote atapatikana kuwa amekula mali ya mwananchi ikiwa ni hakimu anawezakushitakiwa.

Kuna judiciary commission, mtu anaweza kushitikia, kuna hivi sasa, law society of Kenya, kwa njia jizi mtu yeyote, mwanasheria yeyote ambaye atatambulikana kuwa amekula pesa za yule customer, wake au client wake anaweza kushitakiwa. Na wewe ukiwa mwananchi pia unaweza kushitaki, there is a public protector. Na the public defender, all these institutions .....(Inaudible) hizi tumeziweka, kwa hivyo lazima tutakuwa na njia moja au njia mbili, ambayo mwananchi inaweza kuitumia kupata haki yake. So, it is just up to the worker to take that legal action and the man is right, and na tume-make sure that zile organizations ambazo zahusika kama vile.....(Inaudible) yule, wakili ambayo yuala pesa za clients waache, wale huduma yake na kadhalika. So, that is something that can be dealt with in my view.

Kuna njia yaani, kumujuwa au kumtambuwa yule ambaye amekula pesa za mwananchi, na hakumpeleka mahakamani, na hajui mahakama, so, that is why we want to clear or clean the whole judicial system. Na njia tutapata taabu na baadhi ya mahakimu kwa kuwa tumesema kwamba kuna haja hapa ya kusafisha, kutumia kifagiyo, kuondoa wale ambao hawatoi huduma inayopasa kwa hayo maneno. So, they .....(Inaudible) or there could be a rebel for that sort of thing.

Nisha taja commission for human rights under .....(Inaudible) of justice. Tuna picha hapa sijui kama mliiona page 68, mtu anaweza kushitaki kule, lakini inategemea ikiwa hii Katiba itakubliwa, that only time when that commission, will be coming to operation, commission hii au Tume hii haiwezi kuwekwa mpaka tukubali hii Katiba.

Na Bwana Bakari Salim umesema kwamba huu ni mswada mzuri wa Katiba lakini wako wengine ambao wajaribu, .....  
*End of side of Side \$\$\$\$\$* kusema hii tunaipenda, wananchi wenyewe kuwatumia wajumbe wao na waakilishi wao katika huu mkutanao mkubwa wa wa national conference na kuwaambia wasikubali ila Katiba hii ipitishwe, Hatusemi kwamba ni nzuri a hundred percent, sisi wenyewe tuliandika. Kama nimesema hapo awali hatuna, sisi si wale genius wenye akili zaidi kuliko wenzetu, la Commission, na hiyo conference lazima iwe ifikirie jambo hili. Lakini ikiwa wananchi wengi zaidi, majority wamependelea. Na inshalalah katika huo mkutano mkubwa itakuwa bora zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. Na muhimu ni kwamba mtu aitetee, kama yeye binafsi kuhudhuria mikutano naamini kwamba hivi leo kutakuwa na, kulikuwa labda asubuhi sijui, hatajapata habari. Kulikuwa na maandamano Nairobi, kui-support hii Constitution, na mawakili pia na kadhalika.

Ni jambo la kufikiriwa na wananchi, sisi hatuwezi kufanya jambo lolote, tumeeandika tumesema, sisi wananchi wametokea wakaja hivi na hivi, tumeandikwa vile. Na sasa ni tegemeo kwa raia mwenyewe kutusaidia naona mwenzetu hapa Bwana Philo umevaa ile ribbon, yellow, na ndugu yetu mwingine amevaa, hiyo ni ishara na wengine hapa. Nimefurahi sana kwamba tuna support kwa jamaa wengi sana. Na Mungu anisaidie kwa ajili ya raia na wananchi na ndugu zetu zinaweza kuendelea kwa .....(Inaudible).

Kwa hakika nafikiri Bwana Musa Mohammed umesema kwamba, tuna ardhi lakini twaendelea kulipa kodi, nafikiri nilijibu swala hilo awali. Utalii, faida ya utalii hatupati, pia tumependekeza katika taarifa yetu, kwamba faida yeyote inayopatikana au mali ya asili ya wananchi, nilisema hapo awali mapema sana, kwamba katika mambo ya bill of rights, na pia maadhili yetu, tumesema kwamba ya asili igwanywe kwa njia iliyo adilifu, ili kwamba asiweko mwananchi au eneo la nchi ambako jamaa wasema kwamba angalia pesa zote zaenda kule. Beyond that stage, hiyo itakuwa ni detail sasa. Lakini nataka kwamba, tuseme faida ya utalii, iwafikie wale ambao wanashugulikia utalii, au eneo kama la Pwani ambalo faidika kwenye utalii lipate sehemu fulani.

Na hapo pia kuna commission maalum itakayofanywa ambayo itahakikisha, kwamba grants au pesa kutoka Nairobi zitafikishwa katika maeneo ambayo haikupata faida ya kutosha kutoka mapato kama hayo. Swageni, ikubaliwa hiyo, itakuwa ni kazi ya Tume ambayo itafanyika, na kazi ya Serikali za district kudai kazi kama hizo. Mombasa district council, kwa mfano itasema kwamba sisi twahitajia pesa nyingi zaidi kuliko nisema district yote nyingine. Maana mapato kutoka utalii, Mombasa ni nyingi zaidi. Na hii inahitaji ile grant itakayotoka Nairobi kufika hapa Mombasa district. Na mambo ya mpango tu kufanywa sasa, lakini tumetoa mapendekezo ya kutosha ambayo itasaidia katika kuongoza commission, kuongoza district, kuongoza serikali ya kati, wa central Government kufanya kazi yake. Maana kutia details zote katika desturi au katiak Katiba, haiwezekani, itakuwa Katiba kubwa sana, lakini hii Katiba ni law, representative law, is supreme law, na kisha kuna law nyingine kama tulivyo kufanywa kuhakikisha kwamba mambo itafanyika.

These are some, Mazrui Land Trust, tumesema kabla nafikiri hujafika .....(Inaudible) utaondoka. Tumesema kwamba

kutafanywa uchunguzi katika malalamiko ya ardhi, na akiwa ardhi imepatikana kwa njia isiyo sawa, sisemi kwamba ni ya Mazrui land peke yake, lakini kuwa, mamalamiko yoyote juu ya ardhi yatafanywa uchunguzi na ikiwa kumetokea hitalifu yeyote, basi itatuliwa na Serikali. Hii Mazrui Trust Land ina historia ndefu, inarudi nyuma kufikia nineteen something, na kuna historia nyuma yake, na lakini kuna pia taarifa, documents na kila kitu ambacho kimewapa hiyo haki. Chini ya sheria mtu akipewa haki na kama title haitakuwa rahisi kumpokonya haki yake. Hivi ambavyo nimesema. Maana mkisoma, au nikisoma mimi nitawasomea habari ya title deed,

**Audience:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Hebu nisome kidogo, kwa hivyo kama nimesema ana title deed, huenda akafanywa uchunguzi, alipata vipi hiyo land, na ikwa ardhi imepewa kwa njia isiyo halali, kama nimesema hapo awali, ardhi itapokonywa. Na kama nisemavyo, Mazrui Land Trust, imepewe pia karatasi zake, na documents zake, ndio kesho mahasimu hizo si halali, mambo itabadilika, lakini hatuwezi kusema kwamba Mazrui Land Trust leo au kesho lazima iondoshwe. Lazima kufanywe uchunguzi kwanza, mara kila mtu ambaye anasideline title deed, title ikiwa any times tutaibadilisha au kumpokonya mtu title deed yake italeta matata makubwa sana. Ni mambo ya kuchunguliwa, na kutakuwa miaka miwili chini ya Katiba hii, uchunguzi huo ufanywe, na kesi imalizwe katika muda wa miaka hiyo.

Mwana Kombo umekuja mbele ukazungumza habari ya majimbo, na wataka majimbo tu Nafikiri kabla hujaja, nilieleza jinsi ambavyo majimbo ilikuwa ni taabu kuitia kwenye Katiba. Nilieleze sababu, sababu sisi kutaka majimbo nilieleza, tukasama kwamba, sababu hizo za majimbo au za kutaka majimbo, sasa tumezitimiza kwa njia ya wilaya. Maana mama Mwana Kombo, tulitaka majimbo, jamaa wanaotaka majimbo kwa kuwa Serikali iko mbali sana, haitujali, haijui maslaha yetu. Twataka watu wenyewe watuhukumu.

Kwa hivyo tumetia Serikali ya wilaya, kwa hivyo Mombasa pekee yake, au Kwale peke yake, kutakuwa na baraza la kuendesha Kwale district au wilaya ya district, na hapo kodi katika eno hilo la Kwale au eneo la Mombasa, litakusanywa, na pesa hizo zinatumiwa pale pale. Pesa hizo zitatumiwa kuwapa watu wa Kwale au watu wa Mombasa huduma wanoitaka. Huduma ya elimu, shule, huduma ya matibabu, clinics na hospitali na kadhalika, huduma ya bara bara, mengi ya watu kutaka majimbo ili wapate huduma siyo? Sasa huduma hizo, wacheni kupewa ustawi wa jimbo nzima. Tuseme jimbo la Pwani, tumependekeza kwamba wapawe watu kwenye district yao, wilaya yao peke yake. Pia ni majimbo haya, siyo? Lakini majimbo kwa udogo zaidi. Na hapo kutapa huduma zaidi maanake pesa za Kwale zitatumiwa pale pale Kwale district. Pesa za Mombasas zitatumiwa pale pale Mombasa district, kodi zile.

Na kutakuwa na baraza ambayo itafanya kazi ile ya pale pale, watu wa Kwale, baraza yao, district council yao, watafanya kazi ya kustawisha eneo la Kwale. Na kwa hivyo, mhimu ni utumishi kwa mwananchi, kwa hivyo kila mwananchi atatumikiwa na district council yake, Serikali yake ya district, inaitwa Serikali ya wilaya, badala ya serikali ya majimbo.



**Ms. Mwana Kombo:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Lakini sasa ikiwa watu wenyewe hatutumikii uzuri, usemavyo wewe, nani atakaye tumikia watu wa Nairobi? Au watu wa Kisumu, watu wa Nakuru?

**Ms. Mwana Kombo:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Basi ni hivyo nilivyo sema kwamba hapa hapa tutachaguwa watu ambao twajuwa kuwa wanaweza kufanya kazi. Na wasipofanya kazi, hawa hawatakaa milele, baraza la serikali ya wilaya itakuwa na baraza lake, kama vile, tuseme kama bunge la wilaya, nyinyi mtawachaguwa.

**Ms. Mwana Kombo:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Basi mtawachaguwa tena, mchaguwe uzuri, makosa ni yenu kwamba mwachaguwa watu labda ambao hawafanyi kazi ipasavyo. Kwa hivyo hapo ile system ya choice ni juu yenu, na usipofanya kazi mtaondoa. Waje wengine ambao ni bora zaidi.

**Ms. Mwana Kombo:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Nafikiri, ningesema hivi, Mwana Kombo, inshala tutapata nakala ya taarifa yetu hii, kwa Kiswahili hivi karibuni. Na utaisoma uzuri ifahamu, maana muhimu zaidi kwa mwananchi, tuonavyo sisi ni kuwa hatukupata huduma. Watu wataka majimbo kwas kuwa wanasema kwamba kukiwa na jimbo letu wenyewe, tutaliendeshe sisi wenyewe watakuwa na watu wetu, watu wetu watakuwa na imani zaidi, watu wetu ndio watakao hudumiwa na kutupa utumishi bora zaidi. Kwa hivyo tumesema kwamba kutakuwa na maadili ya jimbo nzima la Pwani, kuwa na wilaya kadha wa kadha pwani. Kisha tukisama kwamba kila wilaya, itajiendeshea maisha yake, yenyewe, kupata pesa, kustawisha bara bara, kujenge skuli, na shule, na kadhalika, na kuleta maji katika eneo lile lingekuwa na haja ya maji siyo? Kisha, wilaya mbili, tatu zitaungana pamoja kusaidiana. Kwale tuseme na Mombasa, na Malindi watashirikiana au Kwale na Mombasa. Kilifi na Malindi watashirikiana kustawisha eneo la Kilifi na Malindi pamoja.

Na kisha Serikali ya kati au central Government wana wajibu chini ya hii Katiba kuwapa pesa zaidi ikiwa mwahitajia ili kustawisha eneo lenu. Na muhimu ni maendeleo, tunataka maendeleo siyo?

**Audience:** Ndio

**Com. Prof. Salim:** Lakini si muhimu, ikiwa ni majimbo au Serikali ya majimbo, Serikali ya wilaya na kadhalika, muhimu zaidi ni maendeleo na utumishi kwa mwananchi. Kama nilivyosema hiyo ni, hilo ni pendekezo letu, utasoma, na je, utafurahi, utamshika Bi Amina pale ambaye atakuja kule Nairobi katika mkutano huo mkubwa, umwambie kwa nini hutaki Serikali ya wilaya wataka majimbo. Na ukimbembeleza akikubali, lakini mwingine atamwambia la, afadhali tufwate Serikali ya wilaya. Kwa hivyo yote haya itajadiliwa ishala. Shukrani sana,

**Ms. Mwana Kombo:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Na kama nilivyosema kwamba wale ambao mtawachaguwa ikiwa ni katika Bunge au kokote, au hata Rais ambaye mtamchaguwa, hatakaa milele pia. Mjumbe wa Bunge amepewa miaka kumi kutosha kabisa kabisa, mwaweza kumtoa baada ya miaka mitano mkitaka, lakini akiingia tena kwa miaka mitano mingine, na akimaliza miaka mitano mingine, hawezi tena kusimama. Ataingia mwingine mwenzake.

Rais pia amepewa muda wa miaka kumi maximum, mwisho kabisa miaka kumi, ataingia mitano kwanza, kisha akitaka atasimama tena, mkimuingiza, miaka tano mingine, ikimalizika miaka mitano mingine, anaondoka anakuja mwingine. Kwa hivyo hii ni demokrasia ambapo mtu siyo hatoi huduma inayopaswa kutoa, raia ndiye anayo haki ya kumuondoa. Na kuna njia tumeleza jinsi ya kumuondoa mbunge pia. Sikumuondoa kwa kumpigia kelele na kumfukuza, kwamba kuna procedure katika ile eneo lake au constituency yake, idadi maalum ya wale waliojiandikisha, kupiga kura lazima wapeleke ombi la kumuondoa. Na ombi hilo litapelekwa Bungeni kwa speaker. Speaker atafanya committee yake kufanya uchunguzi, je, ni kweli huyu, amefanya kazi mbaya na kadhalika. Ikiwa imethibitishwa, kutapigwa kura na atabadilika, la akiwa ni, fitina tu, wajuwa jamaa wengine kazi yao ni kufitini tu, na kuzusha kila aina ya haki zetu. Kwa hivyo lazima uchunguzi ufanywe katika malalamiko yoyote sawa.

Tuna maelezo mengi, kwa hakika hatuna wakati tutapitia sasa kuwa saa saba unusu, kuna sala ya aduhuri kwa ndugu zetu. Waislamu kuna chakula kupikwa, akina mama waenda kulisha watoto na kadhalika, lakini nimefurahi sana kuwa mumekuja kwa wingi, na ningewahimiza mjaribu kupata nakala ya Consitution. Wale waliyo na magazeti ya Nation na kadhalika, mpatie mwenzako jirani yako apate kusoma ili mwenyewe mpate copies kwa kituo chetu ndio, na baada, na wale ambao hawawezi kuona, kwa hivyo hawezi kusoma, karatasi kama hizi zetu, tumechapisha braille, tumeandika kwa lugha ya wale ambao hawawezi kuona ili waweze kusoma yaliyomo pia. Na, anything else?

**Speaker:** .....(Inaudible).

**Com. Prof. Salim:** Na bali na hayo, kama nilivyosema kwa hakika kuwa twashukuru sana, tumefurahi sana kuja hapa leo, natumai kuwa tumefahamiana, sana, mtaendelea kujadiliana wenyewe kwa wenyewe juu ya hii Katiba na kuwashawishi wale

wajumbe ikiwa ni mjumbe wenu ma-MP pia msemi naye mumwambie fikira zenu na jinsi mnavyofikiria. Mzee, kwa hakika tume,

**Speaker:** Swali moja tu tafadhali.

**Com. Prof. Salim:** Ah, karibu, ya mwisho jamani, nampa, ameniomba lazima nimpe.

**Mr. Mohammed Abdula Magathu:** Mimi nina swali moja, ningesema mengi lakini sasa sisemi kwa sababu ya kufaheshima, kwa sababu ya kufanyia heshima, mimi nina swali moja, linaniumiza sana. Kuna watoto wa Kiislamu wanaenda school asubuhi saa mbili, na wakitoka school saa saba, saa saba wakija nyumbani saa saba unusu warudi school, na pia saa kumi wasoma moja kwa moja mpaka saa mbili za usiku, unaona pale? Sasa mimi haya mambo yaniumiza sana. Mimi nishamaliza kusomesha watoto wangu lakini yaniumiza, kwa sababu wale waislamu, twataka wasome, saa kumi, .....(Inaudible)

Two, siku ya Jumamosi wawe nyumbani. Jumapili, wawe nyumbani, wawe wanaendelea na madrasa. Mungu mwenyewe alisema, .....(Inaudible) elimu ya kizungu ni dunia. Hili mwenzini ndilo ambao tatahukumiwa nalo kesho, wakera bwana. Watoto wetu twataka uiandike hicho kitu, siyo kuniambia naam .....(Inaudible) iandike bwana maana huu ukweli kwani mimi .....(Inaudible) nilikuwa nina mengi, na ungefurahi lakini si neno, maana muda ule wa kwanza, nilikuja mkayasema, maana ilikuwa matatiso mengi, lakini, I am sorry.

**Com. Prof. Salim:** Asante sana kwa maoni yako, na twakushukuru na sasa ningependa neno la mwisho, kumpa yule niliyemtaja hapo awali, mmoja wa waakilishi wa Mombasa district, Bi Amina Rajab Suber, kwa dakika moja tu Amina.

**Bi. Amina Rajab:** *Asalam Aleykum* ndugu zangu, baba zangu na mama zangu, mimi ni Amina Rajab Suber, ni ndugu, mtoto wenu, ni mwenzenu, nafikiri wengi hapa mwanifahamu. Mimi ni Mmiji kenda mwenzenu, ingawa hatutaki ukabila, sasa, lililofahamishwa hapa Bwana Salim ni lile shitaka la jana. La kwamba wanawake tuko kidogo, sasa nilikaa nyumbani nikafikiri, nikaona labda ni hii .....(Inaudible) ambao tutafanya mikutano yetu, akina mama wengi huwa wako nyumbani saa hizi, wapika, watazama watoto, labda ndio sababu wakashindwa kuhudhuria hii mihadhara yetu. Sasa nilikuwa ninaombi, watume kupitia kwako Bwana Chairman. Kama kutakuwa na kikao cha pili, kama walivyo ahidi, basi tafadhali tungeomba labda tuweke wakati wa mchana. Kipindi cha saa tisa labda hivi, itakuwa ni wenzetu washamaliza kazi ma nyumbani, kwa sababu wanawake wamechangia mengi sana kwenye Tume hii, kwenye Katiba hii. Kwa hivyo tungependa na hao leo wasikie yale yaliyoko, ili tuweze kujua wamekubaliana nayo ama la, yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Prof. Salim:** Asante Bi. Amina kwa wazo lako nzuri na tumezungumza juu ya jambo hili kama nilivyosema, na tunajaribu kupanga mikutano miwili mitatu, zaidi, na itategemea jinsi ambavyo district coordinators, .....(Inaudible) watakavyo panga, na inshala watafaulu katika kufanya mpango huu wao, shukran kwa wazo lako. Na kwa hayo, tunamaliza, wakati umekuwa mrefu

lakini ni mzuri, kwa upande wetu tumefaidika sana hapo, kukutana nanyi, na kupata maoni yenu juu ya tuliopendekeza. Tuombe kwamba mwishowe, raia wa Kenya, kila raia wa Kenya, atafanikiwa apate Katiba ambayo inastahili, mabadiliko kuna haja ya kuyafanya, na inshala kutakuwa na mabadiliko ya heri na ya amani. Tubadilishe nchi yetu iwe moja, lakini wakati huo huo tuheshimiane, tusaidiane, kuijenga zaidi, nchi yetu, kama .....(Inaudible) yetu sote. Shukran na ningemaliza zaidi kwa dua, ningemuomba mwenzetu atu fungie kikao chetu kwa dua, Sheikh.

**Mr. Sudi Mwakama: *Prayer in Arabic.*** Katika mkutano huu tuliyo yazungumza yakakubaliwe kule mbele. Jinsi tuliyazungumza hapa yabakie hapa .....(Inaudible) yakawa hayapatikani, tunaomba Mwenyezi Mungu utujalie katika Tume hii, watu wako mbele na hawa, washirikiane, ili utuwezeshe kuyapata mabadiliko yetu. *Arabic.*

**The meeting closed at 2.00p.m. with a prayer.**